# Nipashe

Jumanne Mei 19, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580235

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
SAYANSI
NA GAUDENSIA MNGUMI
Kiama madhara ya simu za mikononi uhai, mazingira- 2

UKURASA 11



## Kesi Shamim na mumewe tuhuma dawa kulevya Mei 25

UKURASA 3

# Ndugai, Mbowe mnyukano mkali

• **Spika** akosoa kauli vifo vya corona, atabiri kigogo huyo wa Chadema kutorejea bungeni mwaka huu...*Endelea ukurasa 2*



### BAA LA CORONA

**Unapokuwa nyumbani kujilinda na ugonjwa wa Covid-19, jaribu kupunguza kukaa muda mrefu sehemu moja, kama unafanyakazi ukiwa umekaa, unasoma, unaangalia TV au kuangalia mitandao ya kijamii na michezo ya kompyuta, chukua breki ya dakika 3 -5 kila sekunde 20 -30 kusimama na kujinyoosha. WHO**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**

## Masharti 8 malori Rwanda, Tanzania

UKURASA 3



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakinunua mbuzi katika mnada wa Vingunguti, jana, ambapo bei ya kitoweo hicho, ilionekana kupanda kuelekea sikukuu ya Eid El Fitr kutoka Sh. 80,000 mpaka 100,000 za awali, kwa mbuzi mmoja hadi kuanzia Sh. 100,000 mpaka 140,000. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


## Tanzania yafungua anga, watalii watakiwa vyeti corona

UKURASA 2


MICHEZO TAKUKURU: WATAZITAPIKA FEDHA ZA JPM UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Tanzania yafungua anga, watalii kuja na vyeti vya corona

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imetangaza mwongozo mpya utakaosimamia sekta ya utalii nchini katika kipindi hiki cha vita dhidi ya janga la virusi vya corona unaomtaka kila mtalii anayeingia nchini kuwa na ushahidi wa cheti kinachothibitisha kuwa amepimwa na hana maambukizo ya virusi hivyo.

Vilevile, imetangaza kufunguliwa kwa anga la Tanzania kuanzia jana kwa ndege zote za kibiashara, misaada, kidiplomasia, za dharura na ndege maalum.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangwala, alitangaza mwongozo huo mpya wa sekta ya utalii alipozungumza na vyombo vya habari jijini hapa kuhusu kurejea kwa shughuli za sekta ya utalii nchini hivi sasa.

Dk. Kigwangwala alisema kuwa kutokana na Rais John Magufuli, kutangaza kufungua usafiri wa anga nchini pamoja na kuondoa masharti ya kuwaweka karantini, watalii kwa siku 14, kumetoa fursa ya sekta hiyo kurudi rasmi nchini.

"Tunamshukuru Rais Magufuli, kwa kufungua anga letu na kuanza kupokea ndege kutoka nje pamoja na watalii kutoka mataifa mbalimbali kuanza kuingia nchini katika utaratibu maalum," alisema Dk. Kigwangwala.

Pia, alisema kutokana na serikali kurudisha sekta ya utalii katika hali yake ya kawaida kama ilivyokuwa awali wameweka miongozo ambayo itasaidia kusimamia kwa wakati huu wa janga la corona.

Alisema moja ya mikakati ni kuhakikisha kuwa watalii wote wanaoingia nchini wakati huu, wanakuja na ushahidi wa vyeti vyao ambavyo vinaonyesha wamepima na hawana maambukizo ya corona.

Pia, alisema watahakikisha kuwa watalii wanaoingia nchini hawaambukizwi virusi vya corona pamoja na kutoka kwa wananchi watakao wahudumia ili kila mmoja abaki kuwa salama katika kipindi chote watakacho kuwa nchini.

"Kila mtalii kulingana na hali ilivyo atakayeingia nchini lazima aje na ushahidi wa cheti ambacho kitaonyesha kuwa amepima na kuthibitika kuwa hana maambukizo ya virusi vya corona," alisema.

Alisema kuwa kutakuwa na utaratibu wa kupima virusi vya corona wahudumu watakao kuwa wanaongoza watalii pamoja na watumishi wote wa viwanja vya ndege ambao watatengamana na wageni wote watakaoingia nchini.

"Kampuni ambazo zitahusika kuhudumia watalii serikali itazipatia cheti maalum cha uthibitisho kuwa zinavyo vigezo vya kuhudumia watalii hao," alisema.

Vilevile alisema migahawa, hoteli pamoja na kampuni zote zitakazo husika katika kuhudumia watalii watu wake watatakiwa wote kupimwa virusi vya corona na watakao kuwa hawana maambukizo ndiyo watakao hudumia.

"Lakini wahudumu hao wote watakuwa wanafanya kazi kwa shifti na kabla ya kuanza kuhudumia watawekwa kwenye karantini ya siku 14, na watakao bainika kuwa wapo 'negative' ndiyo watakao hudumia watalii kwa muda wa mwezi mmoja baada ya hapo watarudi kwenye familia zao na wengine kuchukua shifti," alisema Dk. Kigwangwala.

Alisema muongozo huo watausambaza kwenye ofisi zote za ubalozi nchini na nje ya nchi pamoja na kwenye kampuni ya mawakala wa utalii.

"Muongozo huu umetengenezwa na serikali kwa kushirikiana na kampuni binafsi hivyo sekta ya utalii nchini itaanza na hakutakuwa na madhara yoyote kwa Watanzania kwa kuwa lengo letu ni kuhakikisha kuwa tunawalinda wageni pamoja na wananchi wetu dhidi ya corona," alifafanua.

Wakati Dk. Kigwangalla akiyasema hayo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alitangaza jana kufunguliwa kwa anga la Tanzania kuanzia jana.

Aliliagiza Shirika la Ndege (ATCL) kujipanga kurejesha huduma za usafiri katika nchi zilizofungua anga zao au zinazohitaji huduma zake.

Waziri Kamwelwe alitoa kauli hiyo alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema ndege hizo zinaruhusiwa kuruka, kutua na kupita juu ya anga na kwamba hatua hiyo imechukuliwa kufuatia kufanyika kwa tathmini ya mwenendo wa ugonjwa wa corona.

Alisema Mei 7 mwaka huu, serikali iliweka zuio kwa ndege za abiria za mashirika ya ndege ya kimataifa kuingia nchini, zuio lililotokana na kuongezeka kwa kuenea kwa mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Alisema zuio kama hilo liliwekwa nchi nyingi duniani na lilikuwa ni sehemu ya mkakati wa kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo baada ya kubainika kwamba usafiri wa anga unachangia kwa kiasi kikubwa kuendelea virusi hivyo.

"Baada ya tathmini ya mwenendo wa ugonjwa huu hapa nchini, kama ilivyotolewa na Rais John Magufuli jana, imebainisha kuwa udhibiti wa ugonjwa huu kuendelea kuimarika na kuwa wagonjwa wamekuwa wakipungua katika vituo mbalimbali," alisema.

Kamwelwe alisema pamoja na hatua hiyo, serikali itachukua taratibu zilizowekwa na Shirika la Afya Dunia (WHO), Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, zitazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha abiria wote watakaoingia au kuondoka ndani ya nchi wanapimwa joto na endapo watahisiwa kuwa na viashiria vya corona, watawekwa sehemu maalum kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

"Endapo abiria yeyote atabainika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona, taratibu za kiafya zitachukuliwa," alisema.

Kuhusu ATCL, alisema wizara inatambua kuwa kufunguliwa kwa huduma ya usafiri wa anga Tanzania kutarejesha fursa nyingine za kibiashara katika baadhi ya maeneo hususan yale yaliyokuwa yanahudumia watalii.

"Hii ni pamoja na mashirika yanayosimamia mbuga za wanyama, hoteli na kampuni zinazohudumia watalii, hivyo zichangamkie fursa hiyo huku mkizingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu Covid-19 ikiwa ni pamoja na matumizi ya barakoa na vitakasa mikono," alisema.

Waziri huyo pia aliiagiza Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) kulitaarifa Shirika la Anga la Kimataifa kuhusu uamuzi wa kufungua anga.

"Pia, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) pamoja na kampuni ya kusimamia na kuendeleza Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO) wahakikishe wanajipanga vyema wakishirikiana na Wizara ya Afya kuhudumia ndege mbalimbali zitakazoingia nchini ikiwa ni pamoja na ndege zitakazobeba watalii," alisema.

***Imeandikwa na Augusta Njoji na Paula Mabeja***

# Spika na Mbowe mnyukano mkali

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

SIKU moja baada ya Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, kumtuhumu Job Ndugai kwa mambo mbalimbali, Spika huyo wa Bunge, ameibuka na kumjibu.

Juzi, Mbowe akilihutubia taifa kupitia njia ya mitandao ya kijamii, alikosoa vikali Bunge kushindwa kuchukua uamuzi wa kuwapima wabunge kama wana maambukizo ya virusi vya corona na kutopitisha bajeti wala mpango wa kupambana na ugonjwa huo.

Mbali na hilo, Mbowe pia alisema Spika Ndugai amekuwa akitumia majukwaa ya kitaifa na kimataifa kumdhalilisha yeye binafsi (Mbowe) na wabunge wa Chadema kwa lugha zisizo za staa.

Kiongozi huyo wa Kambi Rasmi Bungeni na Mbunge wa Hai, alisema kuna haja Watanzania kumwombea Spika Ndugai, ili awe kiongozi bora, akidai kuwa kwa sasa anafanya mambo ambayo hayana tija kwa taifa.

Kauli hiyo ya Mbowe imeonekana kumkera Spika Ndugai ambaye jana alikutana na waandishi wa habari bungeni jijini hapa na kusema: "Ninamshauri Mbowe, baada ya kiongozi wa nchi kuzungumza, ni busara angekaa kimya, kuzungumza baada ya Rais kuzungumza, maana yake ni kujipima ubavu na Rais."

Spika Ndugai alisema Mbowe ana uwanja mpana wa kueleza jambo lake akiwa kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni kulinganishwa na wabunge wengine.

Alisema Mbowe ni mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge, mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Kanuni, mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, hivyo anaweza kuwasilisha maoni yake kupitia kamati hizo kuliko kuzungumza kupitia njia zisizo rasmi.

"Ninamsihi aache, ni tabia mbaya isiyofaa, Rais ni kiongozi wa nchi. Ni heshima na hekima, ninamsihi atumie nafasi yake kumshauri Rais kusipovuka mipaka, na sehemu ya kufanya hivyo ni bungeni, au anazungumza haya kwa sababu anajijua hatarudi Bunge lijalo?" Alihoji.

Spika Ndugai alisema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni hupewa nafasi ya kwanza kuuliza swali bungeni, hivyo Mbowe ana nafasi hiyo kushauri, lakini amekuwa mtoro na anapenda kufanya vitu nje ya boksi ambako anamshutumu Spika.

Kiongozi huyo wa Bunge pia alisema wabunge wengi wa Chadema wamesharudisha fedha za kujikimu walizokuwa wamepewa, isipokuwa watatu, akiwamo Mbowe.

"Siyo tatizo wao kutokuja bungeni, tatizo ni kuchukua fedha za umma na kuondoka nazo, ni 'option' yake kujifungia, lakini siyo kuchukua fedha za umma halafu ukazifanyia mambo yako. Wamechukua Sh. milioni 110. Sasa hapo sijui Spika anakosa gani.

"Wamerudisha baadhi, ila yeye (Mbowe) bado hajarudisha, ninamtaka azirudishe na atazirudisha tu, fedha ambayo hakustahili kuchukua ninasema atazirudisha. Ni jambo la haraka, fedha lazima zirudi tu, njia gani? Nitajua mimi, wala msiwe na wasiwasi," alisema.

Spika Ndugai pia alimkosoa Mbowe kuhusu kauli yake kwamba Tanzania kumetokea vifo vingi vya corona na nchi jirani kutokuwa na vifo vingi, akisema: "Nani amemwambia huko hakuna mtu aliyefariki kwa corona? Tukimtaka athibitishe anaweza? Usiidharau nchi yako na viongozi wako."

Kuhusu kauli ya Mbowe kwamba Watanzania wamwombea Spika, Ndugai alitumia maneno ya Biblia akisema: "Ondoa boriti iliyomo ndani ya jicho lako kabla hujaona kibanzi cha jicho la mwenzako."

Spika Ndugai alisema serikali inampatia Mbowe huduma mbalimbali kama vile ofisi, katibu mukhtasi, dereva, gari, nyumba, marupurupu, posho na kipaumbele bungeni, lakini bado amekuwa akiisema vibaya.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akiongoza kikao cha kamati ya uongozi kilichokaa ili kupokea mapendekezo ya mabadiliko ya ratiba ya Mkutano wa 19 wa Bunge nyumbani kwake, Uzunguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

HABARI KITAIFA

# Ushahidi kesi ya Shamim Mwasha, mumewe Mei 25

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa imesema itaanza kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Mei 25 mpaka 29, mwaka huu dhidi ya Abdul Nsembo na mke wake, Shamimu Mwasha.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Elinaza Luvanda, ilitoa amri hiyo jana baada ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Awali, wakisomewa maelezo ya mashahidi, ilidaiwa katika maelezo yake ya ushahidi ya mkaguzi wa tukio kwamba Nsembo alipanda darini akatoka nje kupitia kwenye paa na kujificha nyuma ya tangi la maji juu ya kibaraza.

Upande wa Jamhuri ulidaiwa kuwa na mashahidi 12 na vielelezo wanavyotarajia kutoa ushahidi dhidi ya washtakiwa.

Ulivitaja vielelezo kuwa ni maelezo ya onyo kwa watuhumiwa wote wawili, hati ya ukamataji, ripoti ya uchunguzi wa maabara ya serikali, fomu ya kuwasilisha sampuli maabara, taarifa ya usajili wa gari kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na bahasha zilizokuwa na dawa za kulevya.

Ilidaiwa katika maelezo ya shahidi wa kwanza Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Paschal Daudi, ambaye ndiye alikuwa kiongozi wa upekuzi siku washtakiwa hao walipokaguliwa na kukamatwa, alidai kuwa Mei mosi, 2019 alipewa kazi ya kuongoza ukaguzi katika nyumba ya mfanyabiashara Abdul Nsembo, iliyopo Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa kwa mujibu wa maelezo ya Daudi, walifika eneo la tukio muda wa saa mbili usiku na kugonga geti ambalo lilifunguliwa na mlinzi aliyejitambulisha kwa jina la Bakari Senkokwa na baada ya kujitambulisha na kumweleza kilichowapeleka Senkokwa aliwaeleza wasubiri amuite mwenye nyumba ambaye ndiye mwenye ufunguo.

Kwa mujibu wa maelezo hayo baada ya muda mfupi alitoka mama ambaye alijitambulisha kwa jina la Shamim Mwasha, ambaye alikiri kuwa ndiyo mama mwenye nyumba na mke wa Nsembo.

Inadaiwa Shamim alipoulizwa kuhusu mume wake alisema hakuwa anajua aliko kwa kuwa walikuwa na ugomvi wa kifamilia na hajui angerudi muda gani, lakini wao walimuomba awaruhusu wafanye ukaguzi naye akawaruhusu.

Kabla ya ukaguzi walimruhusu Shamim awakague, alifanya hivyo na kujiridhisha kwamba hawakuwa wamebeba kitu chochote hatarishi kwake.

Walipotakiwa ukaguzi katika maeneo kadhaa hawakufanikiwa kupata chochote wala kumuona yeyote mpaka walipoingia katika moja ya chumba na kukuta vipande vya gypsum vikiwa vimeanguka na alama ya mguu ikionyesha wazi kuwa kuna mtu alipanda darini muda mfupi uliopita.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo wa kutumia simu za mkononi unaojulikana kama 'Mobile Kilimo', utakaowaunganisha wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara kwa njia ya kielektroniki, jijini Dodoma jana. Wengine ni manaibu wake, Hussein Bashe (kushoto) na Omari Mgumba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Makubaliano 8 Tanzania, Rwanda usafirishaji mizigo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TANZANIA na Rwanda zimekubaliana mambo nane ya usafirishaji wa mizigo ikiwamo kuanzia sasa mizigo yote itashushwa katika vituo vya forodha mipakani isipokuwa kwa mizigo inayoharibika haraka na bidhaa za mafuta.

Akizungumza jana jijini hapa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema makubaliano hayo yamefikiwa baada ya kufanyika vikao kwa nchi hizo vilivyokutana Mei 6 hadi 15, mwaka huu.

Alisema hatua hiyo ilitokana na madereva kulalamikia masharti yaliyowekwa na serikali ya Rwanda katika huduma ya usafirishaji.

"Tulifanya kikao na wenzetu wa Rwanda kujadili kwa kina namna ya kutatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuruhusu kendelea kusafirisha mizigo kati ya nchi hizo huku zikichukuliwa tahadhari za kiafya na kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa Corona," alisema.

Alisema wamekubaliana mizigo yote inayokwenda Rwanda itashushwa kwenye vituo vya forodha Rusumo na Kagitumba isipokuwa mizigo inayoharibika haraka pamoja na bidhaa za mafuta kama petroli.

"Magari yanayobeba bidhaa hizo yataruhusiwa kuendelea na safari na yatasindikizwa bure hadi mji husika ndani ya Rwanda, kama mtakumbuka moja ya sharti lililotolewa na Rwanda ni kuwa mizigo hiyo isindikizwe kwa gharama ya Dola za Marekani 500," alisema.

Aidha, alisema jambo la pili, magari yanayobeba mizigo kupita Rwanda kwenda nchini Kongo yataruhusiwa kuendelea na safari kwa kusindikizwa hadi mpaka wa Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC.

"Pia Magari ya mizigo yataruhusiwa kusafiri saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni kwa mantiki hiyo magari hayataruhusiwa kutembea usiku na jambo la nne, taratibu zitawekwa kuhakikisha madereva wanaoshusha au kupakia kwenye vituo vya forodha hawakai muda mrefu katika ushushaji au upakiaji wa mizigo," alisema.

Aliongeza: "Iwapo watalazimika kukaa muda mrefu watapewa maradhi katika hoteli zilizoainishwa kwa gharama za wenye mizigo na hawatapaswa kulala ndani ya magari kwasababu za kiafya."

Aidha, alisema magari yataruhusiswa kusimama kwenye vituo vilivyoainishwa na madereva wote wanaokwenda Rwanda watapimwa Rwanda na Tanzania itawapima kabla ya kuanza safari kwenda Dar es Salaam.

"Saba, unyanyapaaji wa madereva ikiwamo kutoa majina ya madereva waliobainika kuwa na virusi vya corona ni vitendo visivyokubalika, na jambo la nane, kuwe na mawasiliano kati ya nchi hizi mbili kabla ya kuanza kutekeleza kanuni au miongozo yote itakayoathiri biashara mipakani,"alisema.

Aliwaomba wasafirishaji na madereva wa mizigo inayokwenda Rwanda kuheshimu makubaliano hayo na kuwataka kuwasiliana na Wizara hiyo endapo kutajitokeza tatizo la aina yeyote.

Aprili 24,mwaka huu, Rwanda ilitoa tangazo kuhusu huduma za usafirishaji wa mizigo inayokwenda Rwanda au kupitia mpaka wa Rwanda ikitaka mizigo yote kushushwa mpakani, kuwataka wasafirishaji kuwa na madereva wawili (mmoja kutoka Tanzania na mwingine kutoka Rwanda).




**Bonite Bottlers Limited** is delighted to introduce **Kilimanjaro Drinking Water in 6 Litres, 12 Litres and 18.9 Litres.** We have invested in state of the art modern machinery for production of water to enable our customers, consumers and stake holders to get the desired packs for their consumption in homes, offices and in various Institutions.

**AVAILABILITY:-**

- Kilimanjaro Drinking Water in bulk is available at our depots, shops and wholesalers throughout the country.
- For our customers and consumers in Dar es Salaam, you can buy Kilimanjaro drinking water while at home through our online partners for home delivery which are Shoponline Tanzania **www.shoponline.co.tz** and Piki Deliveries **www.piki.co.tz.**

We hope you will continue to support us and enjoy the refreshing taste from the home of Africa's highest peak.

**FOR MORE INFORMATION CONTACT:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar:** +255 754635988 au +255 22 700450/655, **Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

***KILIMANJARO DRINKING WATER IS THE WATER YOU CAN TRUST EVERYDAY!***

# Usajili wakulima kabla ya Juni 30

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imewataka wakurugenzi wa bodi za mazao na taasisi zinazohusika kuhakikisha wanakamilisha usajili wa wakulima wote nchini hadi ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipokuwa akizindua rasmi mfumo wa 'mobile kilimo' uliofanyika jijini hapa jana.

Waziri Hasunga aliwataka wakurugenzi wa bodi za mazao na taasisi zinazohusika kuhakikisha wanakamilisha usajili wa wakulima wote nchini mpaka ifikapo Juni 30.

"Kwa kuwa mfumo huu unazaidi ya mwaka sasa nitumie fursa hii kuwataka wakurugenzi wote wa bodi za mazao na taasisi zinazohusika kuhakikisha wanakamilisha usajili wa wakulima wote ifikapo Juni 30 mwaka huu na kuanza usajili wa mazao mengine," alisema.

Alisema lengo la serikali ni kuwa na takwimu sahihi za idadi ya wakulima wote na aina ya mazao ya kilimo wanachojihusisha kwa kila eneo nchini.

Alibainisha kuwa mpaka kufikia Aprili 2020 jumla ya wakulima 1,275,220 sawa na asilimia 88.1 wa mazao makuu manane ya kibiashara walikuwa wamesajiliwa.

Hasunga aliyataja mazao hayo ni korosho, pamba, kahawa, chai, mkonge, pareto, tumbaku na sukari wameshasajiliwa kupitia mfumo wa kielektroniki wa wizara hiyo.

Aidha, alisema mfumo huo uliozinduliwa wa 'mobile kilimo' ni jukwaa la mawasiliamo linalowawezesha wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara kutangaza na kutafuta masoko kwa kutumia simu ya mkononi.

Aliongeza kuwa mfumo huo uliozinduliwa jana utawawezesha maofisa ugani kutumia mfumo huo kuwasiliana na makundi hayo waliosajiliwa katika maeneo yao ya kiutendaji kwa kutumia simu za mkononi.

Alibainisha kuwa kuna vijiji 12,545, halmashauri 185, wilaya 139 na mikoa 26 Tanzania Bara na uhitaji wa maofisa ugani kwa nchi nzima ni watumishi 21,268 na waliopo ni 7,303, hivyo kuna upungufu wa maofisa 13,961 hivyo wizara imeamua kubuni mfumo huo ili kuondoa changamoto hiyo.

Naye Naibu Waziri Kilimo, Husein Bashe, alisema wizara hiyo mpaka imeanzisha mifumo sita ya kuwahudumia wakulima na wafanyabiashara hapa nchini.

Bashe alitaja mifumo hiyo kuwa ni usajili wa wakulima, utoaji wa vibali, usajili wa wadau wa sekta ya kilimo, ukusanyaji wa taarifa za kilimo, usimamizi na mfumo wa mobile kilimo uliozinduliwa rasmi jana.

# Bajeti sasa kusomwa Juni 11, Bunge kuvunjwa Juni 19

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema bajeti kuu ya serikali itasomwa Juni 11 badala ya Mei 20 kama ilivyokuwa inaonyesha awali.

Pia, amesema Bunge linatarajiwa kufungwa Juni 19 na Rais John Magufuli, badala ya Mei 29 kama ilivyokuwa inaonyesha awali.

Amesema mabadiliko hayo yalifanyika jana baada ya Kamati ya Uongozi ya Bunge kukutana na kufanya kikao cha tathmini za shughuli za Bunge.

Awali, ratiba ilionyesha kuwa bajeti hiyo ingewasilishwa bungeni Mei 20, majira ya saa 10 jioni na Rais John Magufuli angetarajiwa kufunga Mei, 29, mwaka huu.

Vilevile, ratiba hiyo ilionyesha kuwa wizara zingefanya mawasilisho yake, mjadala na kupitishwa kwa siku moja na vikao kuanza saa 8:00 mchana hadi saa 12: jioni.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Spika Ndugai alisema Bunge la 11 litamalizika Juni 19 na kwamba Rais Magufuli ndiye anayetarajiwa kulifunga.

Spika Ndugai alisema mabadiliko hayo yametokana na mabunge ya Afrika Mashariki kuwa na utaratibu wa kusoma bajeti zao siku moja. Alisema kwa sasa bunge la Burundi halipo kutokana na kuwa katika mchakato wa uchaguzi mkuu.

Spika Ndugai alisema mawaziri wa fedha wa nchi za Afrika Mashariki watasoma bajeti kuu Juni 11, hivyo ndiyo mojawapo ya sababu iliyosababisha ratiba kubadilika.

Miswada inayotarajiwa kuwasilishwa na kujadiliwa katika Bunge hilo la Sheria ya Fedha wa mwaka 2020, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2020.

Mengine ni Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea wa mwaka 2020, Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa mwaka 2020 na azimio la kuridhia mkataba wa kimataifa wa utoaji mafunzo na vyeti vya wafanyakazi meli za uvuvi wa mwaka 1995.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Estim, wakiendelea na kazi ya ujenzi wa kituo cha daladala cha Palm Beach katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Upanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Kina Mbowe waiomba korti ikubali rufani yao

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO saba akiwamo Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, wameiomba mahakama ikubali rufani yao na kutengua hukumu ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu dhidi yao.

Vigogo hao waliwasilisha hoja zao za rufani jana kupitia Wakili Peter Kibatala katika Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Jaji Ilivin Mgeta.

Upande wa walalamikiwa uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Fraja Nchimbi, Mawakili wa Serikali Waandamizi, Salimu Msemo na Wankyo Saimon.

Kibatala alidai kuwa walalamikaji wanaiomba mahakama ikubali rufani yao na kwamba hukumu iliyotolewa Machi 10, mwaka huu na Mahakama ya Kisutu itenguliwe.

Pamoja na mambo mengine, alidai hapakuwapo na uthibitisho wa kutolewa kibali cha maandamano na kwamba ofisa wa polisi anayehusika na utoaji wa kibali hicho ni Mkuu wa Kituo cha Polisi Kinondoni (OCD), ambaye hakuitwa mahakamani kutoa ushahidi.

Alidai bila kuacha shaka mashtaka dhidi ya walalamikaji hayakuthibitishwa na walalamikiwa, hivyo hukumu hiyo haina mashiko ya kisheria.

"Mtukufu jaji ni jukumu la upande wa Jamhuri kuthibitisha mashtaka, Mahakama ya Kisutu katika hukumu yake imesema kwamba utetezi haukuweza kutikisa ushahidi imara wa upande wa walalamikiwa, si kazi ya utetezi bali ni ya Jamhuri," alidai wakili huyo.

Alidai kuwa mashtaka yote 12 yaliyowatia hatiani washtakiwa hakuna hata moja yaliyochambuliwa kama mwenendo wa mashauri ya jinai unavyotaka kisheria.

"Mahakama ndio yenye dhima ya kuchanganua ushahidi wa pande zote na kuonyesha mchakato huo kwenye hukumu, lakini katika hukumu hii hilo halijafanyika," alidai Kibatala.

Kuhusu ushahidi wa kielektroniki, wakili huyo alidai ni wa pekee na kwamba ushahidi wa aina hiyo umewekewa vigezo maalum namna ya kuupokea.

Alidai mahakama ilipaswa kupokea kupitia ushahidi wa ziada tofauti na shahidi anaoutoa akiwa kizimbani ikiwamo kupokewa kwa hati katika mfumo wa hati ya kiapo kama msimamo wa mahakama ya rufani unavyoeleza.

Katika hoja nyingine, alidai namna hati ya mashtaka ilivyoandaliwa ilikuwa inachanganya kiasi washtakiwa walishindwa kujua namna ya kujitetea.

Walalamikiwa wengine ni Katibu Mkuu Taifa, John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu-Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Halima Mdee wa Kawe, John Heche wa Tarime Vijijini na Ester Bulaya wa Bunda.

# Zungu ahimiza jamii kutunza mazingira

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, ameitaka jamii kuitumia Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu kutambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari aliyoitoa jana kuhusu maadhimisho ya siku hiyo mwaka huu, Waziri Zungu alisema kitaifa yalipangwa kufanyika mkoani Lindi, lakini kutokana na janga la corona, hayatafanyika.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho haya kitaifa ni "Tuhifadhi Mazingira: Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi", akibainisha kuwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko la matukio ya ukame wa mara kwa mara na mafuriko, chanzo kikuu kikiwa ni uharibifu wa mazingira.

"Mfano wa hivi karibuni, mafuriko yaliyoukumba Mkoa wa Lindi na kusababisha hasara kubwa takriban vijiji 16 viliathiriwa na mafuriko hayo pamoja na watu 19 kupoteza maisha kutokana na mafuriko hayo.

Alisema takriban watu 15,000 wamekosa makazi, huku wakikumbwa na uhaba wa chakula na kuathiriwa na magonjwa mbalimbali ya mlipuko.

"Kaulimbiu hii inahimiza jamii kutumia mbinu mbalimbali za asili na za teknolojia rafiki za kuhifadhi mazingira ikiwamo kilimo cha matone, nishati mbadala, ufugaji wa mifugo chotara na upandaji wa miti ya asili kwenye vyanzo vya maji, ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Waziri Zungu pia alisema kutokana na corona, kila mkoa unapaswa kufanya shughuli za maadhimisho hayo kwa kutumia vyombo vya habari vilivyoko kwenye maeneo yao pamoja na mitandao ya kijamii kwa kuzingatia kaulimbiu hiyo.

"Tuzingatie kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ikiwa ni pamoja na mashindano ya kuandika insha zinazohusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Hotuba za viongozi, ujumbe mbalimbali utakaotumwa kwenye mitandao ya simu pamoja mikutano ya kitaalamu kuhusu mabadiliko ya tabianchi ambayo itafanywa kwa njia ya mitandao ili kujiepusha na corona."

Alisema ni vyema ikafahamika kwamba hifadhi ya mazingira si kazi ya serikali pekee yake, bali ni jukumu la kila mtu katika ngazi zote kuanzia ngazi ya kaya.

"Nitoe wito kwa vyombo vya habari, taasisi zote za serikali na asasi za kiraia tusaidiane katika kuhifadhi mazingira. Watendaji wote katika ngazi zote, hatuna budi kushirikiana katika kutekeleza kwa ukamilifu sheria na kanuni za hifadhi ya mazingira," alisema.

# Kibano walanguzi sukari chawadia

**Na Gwamaka Alipipi,**

DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2020, ambao pamoja na mambo mengine, unaweka sharti la wasambazaji wa sukari kutakiwa kusajiliwa na kupewa leseni.

Akiwasilisha muswada huo bungeni jana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Adelardus Kilangi, alisema marekebisho hayo yana lengo la kuhakikisha kuwa Bodi ya Sukari inasimamia watu wote wanaofanya shughuli zinazohusiana na sukari.

Profesa Kilangi alisema kifungu kipya cha 11b kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya usajili wa wazalishaji wa sukari ambacho ni moja kati ya vigezo vya kupata leseni ya kuzalisha sukari.

Alisema kifungu cha 14 cha sheria hiyo kinarekebishwa ili kuwapa wazalishaji wa sukari jukumu la uingizaji sukari kwa matumizi ya kawaida, lengo ni kuongeza uwazi katika uingizaji wa sukari kwa matumizi ya kawaida.

"Kifungu cha nne kinarekebishwa ili kujumuisha wasambazaji wa sukari miongoni mwa watu wanaotakiwa kusajiliwa ama kupewa leseni na bodi chini ya sheria hiyo.

"Marekebisho haya yana lengo la kuhakikisha kuwa bodi inasimamia watu wote wanaofanya shughuli zinazohusiana na sukari," alisema.

Profesa Kilangi alisema kifungu cha tisa cha sheria hiyo nacho kinarekebishwa ili kuhakikisha kuwa majukumu mahsusi ya mamlaka nyingine yanatekelezwa na mamlaka husika.

Alisema kwa sasa, kifungu hicho kinampa mkurugenzi mamlaka ya kuidhinisha uingizaji mbegu za miwa nchini wakati TOSCI ndiyo chombo mahsusi chenye mamlaka ya kudhibiti masuala yote yanayohusu mbegu nchini.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema kifungu cha 11A kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kupanua wigo wa ushiriki wa wadau katika kupanga bei elekezi za miwa.

"Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuhakikisha kuwa wakulima na wazalishaji wa miwa wanashiriki ipasavyo katika mchakato wa kubaini gharama ya uzalishaji ambayo itakuwa kigezo cha kufikia bei elekezi," alisema.

Alisema kifungu cha 16 kinafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kukiboresha na kubainisha adhabu kwa makosa ya kuingiza na kutoa sukari nchini bila ya kuwa na leseni iliyotolewa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kifungu kipya cha 34b kinaongezwa kwa lengo la kuweka masharti ya ufungashaji wa sukari kufanywa na wazalishaji peke yao. Alisema kifungu hicho kinazuia ufungashaji wa sukari kwa lengo la kubadili jina halisi.

Sheria zingine zilizopitishwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mawakili (Sura ya 341) ambayo sasa mawakili wa serikali hawataruhusiwa kufanya kazi za uwakili wa kujitegemea; Sheria ya Mfuko wa Pembejeo (Sura ya 401); Sheria ya Umeme (Sura ya 131); Sheria ya Mbolea (Sura ya 378); Sheria ya Misitu (Sura ya 323); Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Mifugo (Sura ya 180).

Zingine ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya 1); Sheria ya Taasisi za Kazi (Sura ya 300); Sheria ya Ulinzi wa Taifa (Sura ya 192); Sheria ya Hifadhi za Taifa (Sura ya 282); Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (Sura ya 284); Sheria ya Mbegu (Sura ya 308); na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori (Sura ya 283).



Ofisa ufugaji nyuki Shamba la Sao Hill Mufindi, Said Mboukar (kulia), akiwapa poleni ya nyuki, wanahabari kutoka vyombo mbalimbali vya habari mkoa wa Iringa, ili kuonja, baada ya kutembelea shamba hilo, linalomilikiwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN** .

# Wagonjwa waongezeka JKCI

**Na Romana Mallya**

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Samweli Rweyemamu, amesema tangu ugonjwa wa corona uingie nchini, wagonjwa wameongezeka katika kliniki ya taasisi hiyo.

Dk. Rweyemamu aliyasema hayo jana wakati taasisi hiyo ikiadhimisha Siku ya Shinikizo la Juu la Damu Duniani.

"Wagonjwa waliohudhuria kliniki ya saa 12 asubuhi leo (jana) wameongezeka, tumepata fursa ya kutoa elimu kuhusu vitu vinavyosababisha presha kupanda," alisema.

Aliwataka wananchi kutonunua dawa ovyo mtaani zinazohusiana na kuongeza nguvu za kiume kwa sababu ukizichanganya na za moyo, husababisha madhara ikiwa ni pamoja na kushusha shinikizo la damu na mtu hupoteza maisha. "Ni jambo la muhimu kulielezea ili watu walifahamu kwa sababu linaweza kusababisha madhara makubwa zaidi yanayozidi shinikizo la damu yenyewe," alisema.

Kuhusu madai majani ya chai kusababisha shinikizo la damu, Dk. Rweyemamu alisema hana ushahidi katika hilo ingawa kwenye vitabu imeandikwa yanasababisha mapigo ya moyo kwenda juu sana.

Alisema pengine utafiti unahitajika kufanyika zaidi kuona kama kuna uhusiano na matatizo ya shinikizo la damu.

Kuhusu wenye shinikizo la damu na kuwa na kilo nyingi, alisema mtu wa aina hiyo anaweza kutumia dawa, lakini kama ataendelea kuwa na kilo 150, kuishusha iwe ya kawaida huwa ni vigumu.

"Hili nimeliona nikiwa kliniki, wanakuja wanawake na wanaume wana kilo 150, dawa zote unazimaliza, lakini presha haishuki, inatakiwa mtu kama huyu afanye mabadiliko ya maisha, apunguze uzito wakati akiendelea na dawa," alisema.

Pia aliwatoa wasiwasi wananchi kuwa dawa za shinikizo la damu au za moyo zinazotumika, hazikai tumboni kwa sababu mwili una namna ya kuziondoa.

Ofisa Lishe wa taasisi hiyo, Husna Faraji, alisema utafiti unaonyesha mtu anayefanya mazoezi angalau dakika 30 kila siku, anapunguza uwezekano wa kupata magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza.

"Tunashauri hasa unapokuwa na uzito uliokithiri, lazima uwe na ratiba ya kufanya mazoezi kila siku kwa sababu kufanya mazoezi kunapunguza uwezekano wa kupata magonjwa sugu yasiyoambukiza," alisema.

Alisema wamekuwa wakisisitiza wagonjwa wajue makundi ya chakula, kula kwa kuzingatia uwiano ulio sahihi.

"Tunasisitiza ulaji wa mboga mboga kwenye milo kwa sababu zina faida nyingi za kiafya, pia tunashauri kiwango cha mafuta na aina ya mafuta wanayotumika kuandaa chakula.

"Tunasisitiza matumizi ya mafuta yanayotokana na mimea kuliko yale yanayotokana na wanyama ambayo yana kiwango kikubwa cha rehamu ambazo zinahusishwa na matatizo ya moyo," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ahadi ya serikali kwa wastaafu itekelezwe

**SERIKALI** imewaahidi wastaafu kwamba imejipanga kumaliza kutatua changamoto ya kupata mafao yao mapema kuanzia mwaka ujao wa fedha.

Katika kushughulikia hilo, imesema kuwa imewaweka katika kipaumbele cha kuhakikisha wanapewa mafao yao kwa wakati.

Imesema kuwa imeendelea kufanya uhakiki wa daftari la pensheni kila mwezi kabla ya malipo, kuandaa vitambulisho vipya vya wastaafu vya kielektroniki katika mfumo wa "smart cards" na kuboresha mfumo unaotumika kutoa huduma kwa njia ya mtandao.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ndiye aliyewapa matumaini hayo wastaafu mwishoni mwa wiki bungeni, alipokuwa akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali za wabunge waliotaka kufahamu mikakati ya serikali katika kuhakikisha mafao ya wastaafu yanalipwa kwa wakati.

Katika kutoa majibu ya hoja hizo zilizoibuliwa na wabunge waliochangia katika hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo, Dk. Mpango alisema kinachochelewesha wastaafu kulipwa kwa wakati ni udhaifu katika taarifa, lakini mikakati inaandaliwa ya kuhakikisha wazee waliolitumikia taifa wanastaafu vizuri na kwa amani.

Kwa mujibu wa Waziri Mpango, suala la malipo ya mafao ya wastaafu ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara kuhakikisha wastaafu wanastaafu vizuri.

Alifafanua zaidi kuwa, wizara inawajibika kulipa mafao na pensheni kwa watumishi wa umma, ambao hawachangii katika mifuko ya hifadhi ya jamii, mirathi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio katika mikataba na viongozi wa kisiasa.

Ahadi ya Waziri Mpango kuhusiana na malipo ya mafao wa watumishi wa staafu wa umma kulipwa mapema ni ya pili kutolewa mwaka huu na serikali.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), George Mkuchika, alisema aliahidi kuwa serikali itahakikisha malipo hayo yanalipwa mapema.

Mkuchika alisema wameshabaini kuwa wanaosababisha malipo hayo kuchelewa kulipwa ni maofisa utumishi, ambao alisema wanachelewa kuandaa utaratibu wa kuwalipa, na kuonya kuwa atakayesababisha ucheleweshaji huo atachukuliwa hatua.

Kimsingi, watumishi wengi wastaafu wa umma bado wanaendelea kusotea malipo ya mafao yao, hali inayowafanya waishi katika hali ngumu ya maisha na unyonge.

Baadhi wanalalamikia urasimu kwamba wanapoenda kudai wanaelezwa waende makao makuu ya serikali Dodoma, hivyo kuwapa wakati ngumu, kwa kuwa kwenda Dodoma wanatakiwa kuingia gharama kubwa za usafiri, chakula na malazi.

Kwa ahadi hii ya Waziri Dk. Mpango ya kutatua changamoyo ya muda mrefu ya malipo ya mafao ya watumishi wastaafu wa umma, ni matarajio yetu kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha, hatutawasikia tena wastaafu wakilalamikia malipo ya mafao yao na kuendelea kunyanyasika.

Sisi Nipashe tunaona kuwa Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ndizo zinazohusika katika mchakato wa ulipwaji wa malipo ya mafia kwa watumishi wa umma.

Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa kuwapo kwa utaratibu wa mamlaka hizi kuwa na vikao vya pamoja kwa ajili ya kufuatilia mchakato wa ulipaji wa mafao ya watumishi wa umma kwa wakati mwafaka.

Hatua hii itawezesha kuondoa urasimu, uongo na ubabaishaji wa watumishi wachache wanaokwamisha malipo ya mafao ya watumishi wastaafu, hivyo kuipaka doa serikali.

Kwa jinsi Mkuchika na Dk. Mpango walivyoeleza kuguswa na kunyanyasika wastaafu katika kudau malipo yao, bila shaka watahakikisha kuwa tatizo hilo linamalizika kuanzia mwaka ujao wa fedha, hivyo kuthibitisha kivitendo kuwa serikali ya Rais John Magufuli inawatetea na kuwajali wanyonge.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wananchi wadau muhimu ujenzi miundombinu elimu



Na Sabato Kasika

**NYUMBA** za walimu wa shule za msingi zilizopo nchini ni 41,321 wakati mahitaji halisi ni nyumba ni 222,115, upungufu unaosababisha baadhi ya walimu kuishi mitaani katika nyumba za kupanga.

Serikali inaahidi kuendelea kujenga nyumba za walimu kadri fedha zinavyopatikana, lengo likiwa ni kuboresha mazingira na makazi kwa walimu.

Ndivyo alivyowahi kusema bungeni aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakati huo, Joseph Kakunda, alipokuwa akijibu maswali ya wabunge.

Anagusia kuwa ujenzi wa nyumba za walimu ni jukumu la wadau wote kuanzia serikali kuu, za mitaa na wananchi na akatoa wito wadau wengine kuchangia ujenzi huo.

Sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa nyumba za walimu na ushiriki wa wadau katika kujenga nyumba hizo ni wa muhimu

Juhudi zinazofanywa na serikali za punguza uhaba wa nyumba za walimu linahitaji kuungwa mkono ili walimu wapate makazi.

Upungufu unawalazimisha kupanga mitaani na kukutana na usumbufu ukiwamo wa kutishiwa maisha ambao wangeuepuka kama wangekuwa wanaishi katika nyumba zao.

Mchango wa wananchi ni muhimu kwani utasaidia kila mmoja kubeba sehemu ya ujenzi huo kuliko kuachia upande mmoja na mwisho wake ni kuendelea kuwa uhaba wa nyumba za walimu.

Wadau wa elimu wakishiriki kikamilifu watakuwa wamesaidia kupunguza uhaba huo wa nyumba za watumishi hao wa umma na pia kuwafanya wasitembee na kuchoka kabla hawajafika kazini .

Katika mazingira hayo ya kusafiri au kutembea umbali mrefu husababisha wanafunzi, kukosa msaada wa ziada kwa walimu wanapouhitaji baada ya muda wa masomo kwani kila mmoja anakimbilia kuwahi nyumbani na kuondoka mapema shuleni.

Hivyo ujenzi wa nyumba hizo ni jambo ambalo haliepukiki na linatakiwa kushirikisha wadau wengi hasa wazazi ili kutoa mchango wao katika kufanikisha ujenzi huo.

Kwa mfano wananchi wanaweza kushirikishwa kama nguvukazi wakisomba maji, mawe, kokoto, mchanga na sementi katika ujenzi wa nyumba hizo na kufanikisha jambo hilo.

Siyo hilo tu bali pia inaweza kuweka mipango wakachangia hata fedha kiasi kidogo katika ujenzi huo, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali na kufanikisha ujenzi wa nyumba za walimu.

Ninasema hivyo, kwa sababu ipo mifano ya wananchi katika maeneo mbalimbali ambao sasa wanashiriki katika wa nyumba za walimu wakitoa nguvukazi yao na hata kuchangia chochote.

Mfano mmojawapo ni katika kata mbalimbali za Wilaya ya Musoma, kwa sasa wananchi wanashiriki ujenzi wa nyumba hizo ili kuwatoa walimu katika mazingira ya upangaji.

Hii ni hatua nzuri ya kusaidiana na serikali katika kuikabili changamoto hiyo ya muda mrefu inayoendelea kuwatesa walimu, lakini ninaamini ipo ndani ya uwezo wa jamii ya maeneo husika.

Kinachotakiwa ni kuhamasisha na kuelimisha jamii kutambua umuhimu wa kushiriki katika shughuli za ujenzi wa miundombinu ya elimu kama ambavyo inafanyika wilayani Musoma na maeneo mengine.

Kwa mfano katika Kata ya Bukumi, wakazi wa kijiji cha Buira, wanachanga Sh. 12,000 za nyumba ya walimu huku pia nguvukazi yao ikitumika kusomba mawe, maji, mchango na kufyatua matofaili ya nyumba hiyo.

Wao wameunga mkono juhudi za serikali ambayo imetoa Sh.milioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu wa Shule ya Msingi Buira ulisimama miaka 19 iliyopita.

Leo wanaendelea baada ya sababu za kitaalamu kupatiwa ufumbuzi ili kuhakikisha nyumba inakamilika, ambayo ina vyumba vitatu vya kulala, choo, bafu, stoo na jiko.

Iwapo ujenzi wa nyumba hiyo utakamilika utawapunguzia walimu gharama ya kupanga uraiani au mitaani na pia wakati mwingine inamfanya mwalimu aheshimike ndani ya jamii kuliko ilivyo sasa.

Kwa hiyo kila mmoja ana wajibu wa kushiriki kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu na hasa kwenye ujenzi wa nyumba zao ambazo ni muhimu zijengwe kwa wingi nchini.

## HABARI KITAIFA



Mwakilishi wa kitengo cha Ugavi cha Hospitali ya Mwananyamala, Hiltruda Patrick (kushoto), akipokea matangi ya maji kutoka kwa Geofrey Kivamba wa Brandmiles kwa niaba ya Benki ya Commercial Bank of Africa (CBA) Tanzania, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya msaada wa matangi manane kwa hospitali nne zilizochaguliwa za jiji hilo, kwa ajili ya kunawia mikono, ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona. Katikati ni Mfamasia wa hospitali hiyo, Simon Mbise. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maadhimisho siku ya punda yalivyogeuzwa elimu corona

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Singida kwa kushirikiana na shirika lisilokuwa la kiserikali la INADES Tanzania, wameadhimisha Siku ya Punda Duniani kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu tahadhari juu ya kujikinga na maambukizo ya corona.

Mtaalamu kutoka Idara ya Afya katika halmashauri hiyo, Neema Swai, alisema wadau hao walisaidia pia kutoa elimu kwa wananchi wa halmashauri hiyo juu ya umuhimu wa ufugaji wa punda na matumizi sahihi ya barakoa.

Alisema kwamba jamii kwa ujumla halmashauri imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji, lakini kwa kumtumia punda, wameweza kupata maji tiririka yanayosisitizwa na wataalamu hao kunawa ili kujikinga na ugonjwa huo.

"Mojawapo kati ya mbinu zinazotusaidia katika kukabiliana na hili janga, ni kunawa na majisafi yanayotiririka pamoja na sabuni. Kwa hiyo huyu mnyama punda tunaona katika jamii anasaidia kuchota maji... kwa hiyo jamii inakuwa na uhakika wa kupata maji na wanazingatia umuhimu wa kunawa majisafi tiririka pamoja na sabuni," alisisitiza Neema.

Neema alizitaja shughuli zingine zinazofanywa na punda ni humwingizia kipato mwananchi na kumwezesha kununua sabuni na kumwezesha kusimama katika misingi ya kukabiliana na janga la corona.

Alisisitiza kwamba mwananchi anapopata kipato kizuri kinachotokana na msaada wa mnyama punda, kunakuwa na uwezekano wa kupata lishe au mlo kamili ambao unamwezesha kuwa na kinga nzuri ya ugonjwa huo wa corona.

Ofisa Maendeleo ya Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Adamu Sungita, alisema punda amekuwa msaada mkubwa kwenye maeneo ya vijijini kwani huchota maji ya matumizi ya kawaida na maji ya kuendelea kutakasa mikono kwa ajili ya kujikinga na corona.

Kwa mujibu wa Sungita Halmashauri ya Wilaya ya Singida ina jumla ya punda 7,793, idadi ambayo ni ndogo kufananisha na idadi ya wanyama wengine wanaofungwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Sungita alisema wataendelea kutoa elimu kwa vijiji vingine vilivyobaki ili punda waendelee kutunzwa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Endesh, Kata ya Msange, Joseph Kingu, alifafanua kuwa tangu shirika lisilokuwa la kiserikali lilipoanza kufanya shughuli za mradi wa punda katika kijiji hicho, wameona manufaa yake.

# WFT wadadavua sheria kandamizi wanawake kushiriki uchaguzi mkuu

**Na Mary Geofrey**

MTANDAO wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi chini ya uratibu wa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT), wamefanya uchambuzi wa sheria tano za uchaguzi kwa mrengo wa jinsia kwa lengo la kuangalia vikwazo vinavyowazuia wanawake kushiriki katika uchaguzi mkuu.

Mwenyekiti wa WFT, Prof. Ruth Meena, aliyaeleza hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano kwa njia ya mtandao ili kutoa mrejesho wa sheria walizofanyia uchambuzi kuelekea uchaguzi mkuu.

Alisema lengo la uchambuzi huo ni kutoa muhtasari wa mambo yaliyojitokeza kwenye baadhi ya Sheria za Uchaguzi ili kubainisha mapengo yanayoweza kuwa kikwazo katika kutekeleza azma ya ujenzi wa demokrasia shirikishi kwa mrengo wa jinsia.

"Lengo pia ni kutoa mapendekezo mahsusi yatakayoongoza wadau mbalimbali kuchukua hatua stahiki zenye kukabiliana na sheria za ubaguzi wa aina zote hususani ubaguzi wa jinsia kwenye mchakato wa uchaguzi," alisema Prof. Meena.

Alitaja sheria walizofanyia uchambuzi kuwa ni ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 ya mwaka 2015 na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar namba 4 ya mwaka 2018.

Alitaja sheria nyingine ni ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa namba 4 ya mwaka 1979 namba 292 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 na mwaka 2015, Sheria ya Serikali za Mitaa inayofahamika kama Mamlaka za Wilaya Sura 287 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 na Sheria za Serikali za Mitaa za mmlaka za miji sura ya 288 na mamlaka za wilaya sura ya 287.

Prof. Meena alisema pamoja na sheria hizo, walifanya uchambuzi wa Katiba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zikiwa sheria mama zinazoongoza utunzi wa sheria zote za nchini.

Alisema katika uchambuzi huo waliangazia mfumo wa uchaguzi, haki ya kupiga kura, haki ya kuteuliwa na uwazi kwenye uteuzi.

Alisema waliangazia pia gharama za uchaguzi, uwajibikaji na wajibu wa vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu na kudadavua kasoro zake ambazo ni kikwazo kwa mwanamke kushiriki uchaguzi.

# Askari JWTZ wafundwa ulinzi mipaka na raia

**Na Luteni Selemani Semunyu,** JWTZ

MKUU wa Mafunzo na Utendaji Kivita wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Meja Jenerali Alfred Kapinga, amewataka askari wa jeshi hilo, kuendelea kufanya kazi mama ya ulinzi wa mipaka na raia kwa nguvu zote.

Meja Jenerali Kapinga alisema hayo wakati akihitimisha mafunzo ya porini kwa kuruti kutoka shule ya mafunzo ya awali ya Kijeshi RTS Kihangaiko kundi la 39 yaliyofanyika kwa siku 14 katika pori la Pongwe Msungura, Bagamoyo mkoani Pwani.

Meja Jenerali Kapinga aliwataka kuruti hao kujiandaa kufanya kazi ya ulinzi wa raia kwani kwa kufanya hivyo, watakuwa wanatimiza jukumu la msingi litakaloijenga nchi na kuifanya ikue kiuchumi.

"Kazi mama ya jeshi letu ni kulinda mipaka ya nchi na kuwalinda raia wa nchi yetu, ili waweze kushiriki shughuli za uzalishaji mali kwa amani na kuliletea Taifa tija inayokusudiwa, na kazi hiyo hufanywa na watu imara ambao ni wanajeshi," alisema Meja Jenerali Kapinga.

Meja Jenerali Kapinga aliwasihi kuruti kuendelea kuweka majukumu ya kuilinda nchi, na kwamba mbali na mazoezi, walinde afya zao dhidi ya magonjwa kama corona na Ukimwi.

Aidha, aliwataka wakuu wa vikosi jirani na maeneo ya mazoezi kuyadhibiti maeneo hayo kwa namna yoyote yasivamiwe na wananchi kwani maeneo hayo ni muhimu kwa ustawi wa jeshi.

"Hakuna sababu kwa pori kama hili la Pongwe Msungura Msata kuwaachia raia kwa kuwa tumeshawaachia maeneo mengi na katika eneo hili yapo maeneo mengi... hakuna sababu ya wao kuingia katika eneo letu la mazoezi," alisema.

Aliongeza kuwa eneo hilo licha ya kuwa halijavamiwa kwa ujenzi, lakini wafugaji na wakataji wa miti wachache wameanza kuingia bila kujali kuwa eneo hilo limekuwa likitumika tangu kipindi cha wagombea uhuru kwa mazoezi ya kijeshi.

Aidha, amewataka kufanya mazoezi ya mara kwa mara kuepusha wananchi kuyavamia wakidhani hayana matumizi kwani wakipoteza maeneo hayo hakutakuwa na maeneo mengine.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiondoa matope yaliyokuwa kwenye mtaro yaliyosababishwa na maji ya mvua katika eneo la Vingunguti, jijini humo, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Mbunge Mtulia asimulia alivyougua corona

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Kinondoni (CCM), Maulid Mtulia, amesimulia jinsi alivyougua ugonjwa wa virusi vya corona, na kuwashukuru watu wote waliomuweka katika maombi wakati akipigania maisha yake.

Akizungumza bungeni jana, Mtulia alieleza kuwa alianza kuugua ugonjwa huo Aprili 17, mwaka huu na Aprili 19 alipelekwa katika kituo cha afya cha Mkoze mjini Dodoma.

Alisema kwa sasa amerejea bungeni akiwa na afya njema na anawashukuru Wabunge, Spika wa Bunge, Job Ndugai na Watanzania.

"Nimerudi kwenye Bunge lako, nimepona. Nimekaa kituo cha Mkonze kuanzia Aprili 19 mpaka 13 Mei na kwakweli ushuhuda ninaotaka kuwapa kwa muda wote mimi nilikuwa mtu wa pili, lakini hakujawahi kutokea kifo hata kimoja naungana na Rais John Magufuli kwamba tusijenge hofu kubwa," alisema na kuongeza:

"Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wangu kwani kulipita mafuriko, nimerudi kuhakikisha tunafanya kazi na kuungana na viongozi wangu nikiwa mtu ambaye nina uzoefu, nipo wazi watakapotaka ushiriki wangu nipo tayari kujitolea."

Mbunge huyo alidai kwamba kwa sasa bado kuna unyanyapaa kwa wagonjwa wa virusi vya corona, lakini yeye anashukuru wabunge hawakumnyanyapaa.

"Ugonjwa huu una unyanyapaa, niwaombe wabunge wangu wasiwe na hofu, kubwa... nimpongezee Rais Magufuli kwa kutoa amri kuwa endapo mgonjwa wa virusi vya corona akifariki azikwe," alisema Mtulia. Kwa upande wake, Spika Ndugai alimkaribisha bungeni Mtulia huku akieleza kwamba walimuombea sana wakati akiwa mgonjwa.

"Karibu sana mjengoni, hakika 'tulikumisi' ila tulikuombea sana ulikuwa katika sala zetu tunakuombea.Nawaomba sana Watanzania tupunguze hofu, ugonjwa huu kweli upo, lakini hofu ni tatizo tutulie, wale ambao tutapata majaribu haya tutulie," alisema Ndugai.

# Walilia kituo cha afya kuwanusuru wajawazito

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAKAZI wa kisiwa cha Bezi kilichopo Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza wanakabiliwa na changamoto ya kukosekana kituo cha afya, hivyo kusababisha wajawazito kujifungulia ndani ya mitumbwi.

Aidha, wakazi hao wamesema wajawazito wengine hufariki wakati wa kufuata ng'ambo huduma.

Akizungumzia adha hiyo, Theresia Bernad, mkazi wa kisiwa hicho alisema wanapata tabu wanapotaka kuanza kliniki, kupeleka watoto na kwenda kujifungua kutokana na umbali wa kituo cha afya, hivyo waliiomba serikali kuwajengea ili waweze kupata huduma karibu.

Naye Colnel Fabian, alisema wanahitaji huduma hiyo ili kukidhi mahitaji yao kwa sababu mara kwa mara vifo vinatokea wakati kinamama hao wakiangaikia kwenda kwenye Kituo cha Afya Sangabuye.

"Tupo zaidi ya watu 2,000 katika eneo hili inatakiwa nguvu ya serikali na kuwekeza katika sekta ya afya na kunusuru maisha yetu," alisema Fabian.

Akijibu changamoto hiyo, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Silas Wambura, amewataka wananchi hao kuunganisha nguvu na kujenga boma baada ya hatua hiyo kukamilika wataunga nguvu kwa kumalizia jengo hilo sambamba na kuwapelekea vifaa na wataalamu wa kutoa huduma.

"Nawahamasisha wananchi wa eneo hili la kisiwa cha Bezi wachangie nguvu zao wajenge boma baada ya kukamilisha, sisi kama mkoa tutashirikiana na Halmashauri ya Ilemela na kuhakikisha wanalimalizia hilo boma na kuweka huduma ya afya mahali hapo," alisema Wambura.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amemwagiza mwenyekiti wa serikali ya kijiji wa eneo hilo kuhakikisha wanaanza ujenzi wa msingi wa jengo la zahanati kwa kushirikisha nguvu kazi ya wananchi.

# H'shauri Moro yaanza usafi mazingira shule

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imezindua rasmi kampeni ya kufanya usafi wa mazingira maeneo ya shule na makazi ya watu, ili zitakapofunguliwa wanafunzi wawe kwenye mazingira mazuri ya kujisomea.

Kampeni hiyo ilizinduliwa jana na Ofisa Tarafa wa Manispaa ya Morogoro, Winfred Kipako, Shule ya Msingi Mafisa A, Kata ya Mwembesongo na kwamba kampeni hiyo itawahusisha wananchi wa mitaa yote na kata husika kwa ujumla.

"Kutokana na mazingira ya shule kuwa machafu baada ya kufungwa kwa muda mrefu, tumeamua kuanzisha kampeni ya usafi kwa shule zote za Manispaa hii ili zitakapofunguliwa wanafunzi wakute mazingira mazuri," alisema Kipako.

Kipako alisema kuwa mbali na usafi huo kufanyika maeneo ya shule zote pia utafanyika kwenye makazi ya watu na kwamba kila diwani atakuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wananchi wanajitokeza kushiriki kampeni hiyo muhimu.

Alisema lengo la kuanza katika maeneo ya shule ni kwa sababu shule kwa sasa hazina wanafunzi kutokana na likizo iliyosababishwa na janga virusi vya corona hivyo maeneo mengi ya shule yamegeuka vichaka jambo ambalo ni hatarishi.

Kipako alisema bila kufanya usafi huo maeneo yote ya shule yaliyogeuka vichaka yatakuwa vificho vya wadudu na wanyama wakali ambao wanaweza kuhatarisha maisha ya watoto shuleni.

"Namshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa hii kwa kushirikiana na Ofisa Mazingira kuja na wazo hili binafsi naliunga mkono na nitahakikisha linafanikiwa ili shule zitakapofunguliwa watoto wetu wasome kwa raha," alisema Kipako.

Alisema pia watendaji wote wa kata wana wajibu wa kuhakikisha wanasimamia kikamilifu ili kuleta tija kutokana na umuhimu wake kwa jamii ya wana Morogoro.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheilla Lukuba, aliwaagiza watendaji wa mitaa, kata na maofisa afya pamoja na wananchi kwa ujumla kuichukua kampeni hiyo kwa uzito ili malengo yaweze kufanikiwa vizuri.

Naye diwani wa kata ya Mwembesongo, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji, Ally Kalungwana, alipongeza kitendo hicho na kwamba kampeni hiyo itakuwa suluhisho la usafi maeneo mbalimbali ya manispaa hiyo.

Wananchi wameupongeza uongozi wa manispaa hiyo kwa kitendo cha kuanzisha kampeni hiyo kwa kuwa kutasaidia kuziweka shule ambazo baadhi ya maeneo yake yamegeuka kuwa na vichaka hatarishi kwenye hali ya usafi.

# Apinga wanawake kupuuzwa kwenye nafasi za uongozi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

DIWANI wa Viti Maalumu Halmashauri ya Chalinze mkoani Pwani, Rehema Mno, amesema, hakubaliani na misemo ya kuwa mwanamke hawezi kuongoza, na kwamba mwenye uwezo wa kufanya hivyo ni mwanaume pekee.

Rehema akizungumza na Nipashe jana, alisema misemo ya zamani haitakiwi kupewa nafasi kwa sasa, na kwamba inatakiwa kutumika na wanawake kama fursa katika kuwania nafasi za kuongozi sawa na wanaume.

"Sikubaliani na msemo wa kuwa wanawake hawawezi kuongoza, ninaweza kufanya kazi vizuri na wananchi tukashirikiana katika kuleta maendeleo sawa na kusimamia haki bila kubagua jinsia na makundi maalumu."

Wanawake tuamke sisi ni jeshi kubwa hakuna kuogopa, muda umefika kujipanga na kugombea nafasi za udiwani na ubunge... tusiwaachie nafasi wanaume kuchukua kata na majimbo," alisema Rehema.

Alisema zipo changamoto ambazo amezitumia kama fursa katika kuhakikisha maendeleo yanapatikana katika eneo alilopo.

"Baadhi ya watu wenye ulemavu walikuwa wamekata tamaa baada ya kupata ajali, lakini alifanikiwa kuwahamasisha kuunda vikundi ambavyo walipatiwa mikopo na kuanzisha shughuli za kuwaingizia kipato," alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa wanawake amekuwa akifanya nao vikao vya mara kwa mara kujadili namna ya kujikwamua kiuchumi, na kuwa walifanikiwa kuunda vikundi na kupata mikopo, ambayo wanaendeshea shughuli za ujasiriamali zinazofanya katika hali ya utegemezi kwa wanaume zao.

Mwanaid Selemani na Zainabu Hamis, walisema ni wakati wa wanawake kuungana mkono kwa kuwapa ushirikiano watakaojitokeza kugombea na kuachana na dhana ya kusemana vibaya ili kuongeza idadi ya viongozi wanawake.



Dereva wa bajaj akijaribu kuwapita wenzake mlimani, katika barabara ya kuelekea Kinyerezi, eneo la Kwa Msangi, Mbezi, jijini Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU .**

# Mbaroni tuhuma za wizi wa maji

**Na Neema Emmanuel,**

MWANZA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA) kwa kushirikia na vyombo vya ulinzi na usalama, wamewakamata watu wawili wilayani Nyamagana kwa tuhuma za wizi wa maji na kuyatumia kutumia kinyume cha sheria na taratibu.

Walitiwa mbaroni katika operesheni iliyofanywa usiku wa kuamkia Jumamosi na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Leonard Msenyele, timu yake kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vya Wilaya ya Nyamagana.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kuwa wamekuwa na tabia ya kujiunganishia maji na kuyatumia kinyume cha utaratibu.

Akizungumza baada ya kuwakamata watuhumiwa hao, Mhandisi Msenyele akisema katika operesheni hiyo ambayo walianza saa moja jioni hadi saa tisa usiku katika maeneo ya Nyegezi, walifanikiwa kumkamata mmiliki wa eneo la kuoshea magari la 'You Never Know' ambaye inadaiwa amejiunganishia bomba la maji kutoka kwenye bomba kubwa la Mwauwasa na kupeleka katika kituo chake.

Mhandisi Msenyele alisema mtuhumiwa wa pili aliyetajwa kwa jina moja la Juma, mkazi wa Buhongwa, amekuwa anaiba maji usiku kwa kufungua bomba ambalo linapita kwenye mita na kufunga la kwake na kujaza kwenye matangi kisha alfajiri anarudisha bomba linalopita kwenye mita.

Kwa mujibu wa Msenyele, asubuhi wakienda kukagua wanakuta uniti zinazohesabika ni kidogo tofauti na matumizi.

Amesema, wamebaini mchezo huo mbaya wa watu hao wanaohujumu mamlaka hiyo na kusababisha baadhi ya watu kukosa maji na mbinu zao wamezibaini na kuamua kuanzisha operesheni hiyo.

"Operesheni hii tumeianza leo kuanzia saa moja jioni hadi saa 9 usiku na nimeisimamia mwenyewe na kikosi changu, tumekamata wateja wetu, ambao siyo waaminifu," alisema na kuendelea: "Wamekuwa wakituibia maji na tumewapeleka kituo cha polisi kwa kushirikiana na polisi ambao tumepewa na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Nyamagana."

Pia alisema, operesheni hiyo imelenga kukomesha wizi wa maji katika jiji hilo, kwani wameibiwa sana na watu wamekuwa wakitumia maji sana wakati wa usiku na kuyauza bila kulipa bili kwa Mwauwasa, hivyo kusababishia serikali na mamlaka hiyo hasara na upotevu wa maji.

Aliwaonya wezi wa maji na wananchi kwa ujumla kuwa operesheni hiyo ni endelevu, na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa watakaobainika kuiba maji.

# Tanga waonja neema upatikanaji sukari

**Na Boniface Gideon,** TANGA

UPATIKANAJI wa sukari mkoani Tanga umerejea katika hali yake ya kawaida katika maeneo mbalimbali.

Wiki mbili zilizopita wananchi katika maeneo mengi nchini walikutana na machungu na shubiri kutokana na kuadimika kwa bidhaa hiyo muhimu.

Wafanyabiashara wengi walitumia uhaba huo kwa kuificha kisha kuiuza kwa bei ya juu.

Katika Jiji la Tanga maduka yote ya jumla na rejareja sasa yana bidhaa hiyo, huku tofauti kubwa ikiwa ni kwenye bei.

Maduka mengi ya jumla yanauza kati Sh. 2,900 hadi 3,200 kwa kilo moja wakati maduka ya rejareja yenyewe kilo moja ikiuzwa kati ya Sh. 3,600 hadi 4,000.

Baadhi ya wafanyabiashara wa jumla na rejareja wa eneo la barabara la 15 lenye maduka mengi waliieleza Nipashe kuwa upatikanaji wa bidhaa umeanza kutengemaa, hivyo bei itakuwa inashuka kutokana na mzunguko wa biashara.

Ally Ndahani, alisema mwishoni mwa wiki walianza kupata bidhaa hiyo, lakini ni vigumu kudhibiti bei kwa haraka.

"Huu ni mzunguko wa biashara huwezi kuudhibiti bei kwa haraka, haiwezekani kabisa duniani kote... bei itaendelea kushuka taratibu kutokana na upatikanaji wa sukari kwa mawakala wetu," alisema Ndahani.

Katika mitaa mingi ya Jiji la Tanga hususani maeneo maarufu kama Sahare, Nguvumali, Pongwe Kange, Donge na Raskazone, bidhaa hiyo inapatikana kwa urahisi zaidi huku kilio kikubwa kwa wananchi ni kutokana na bei kubwa ya sukari.

Ashura Kachenje, mkazi wa Nguvumali, alisema wanashukuru kuona hali ya upatikanaji wa sukari kurejea kama awali.

"Sisi tunashukuru kwa upatikanaji, tuliteseka sana wiki mbili hizi, lakini tunaomba bei ipunguzwe ili tumudu kununua, kama unavyoona hapa. Nimetoka kununua hii ni robo nimeuziwa shilingi 1,000 huoni hili ni tatizo," alisema Ashura.

Katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Tanga, bidhaa hiyo imeanza kupatikana ambapo katika wilaya za Mkinga, Pangani na Muheza, sukari inapatikana katika maduka mengi, huku changamoto ikiwa ni bei kubwa kati ya shilingi 3,600 na 4,000.

Katika wilaya za Handeni, Kilindi, Korogwe na Lushoto, hali ya upatikanaji imeendelea kuimarika, lakini bei ikiendelea kuwa tatizo kutokana na kuuzwa kati ya shilingi 3,200 na 4,500 kwa kilo moja hususani katika wilaya za Kilindi na Lushoto.

Katika Wilaya ya Korogwe kilo moja inauzwa kati ya shilingi 2,700 na 2,800 katika eneo la Manundu lililopo Korogwe Mjini.

# Watumishi zaidi ya 11,000 wajiendeleza kielimu




Habari na Augusta Njoji



BUNGE limeelezwa kuwa kuanzia mwaka 2015 hadi sasa, watumishi 11,640 walijiendeleza kielimu katika fani mbalimbali.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Kaliua (UF), Magdalena Sakaya.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema serikali imekuwa ikitoa vibali kwa watumishi kwenda kujiendeleza kielimu ili kuongeza ujuzi na ufanisi katika kazi.

"Je, kwa nini baadhi ya watumishi wanapojiendeleza wamekuwa hawapandishwi madaraja wala kuongezewa mshahara na je, nini mkakati wa serikali kuhakikisha Watumishi wa Umma wanapandishwa madaraja kuendana na Sheria ya Utumishi wa Umma?"Alihoji.

Katika majibu ya ofisi hiyo ilisema watumishi hao waliojiendeleza ni ambao waajiri wao waliwatengea nafasi zao katika Ikama na Bajeti kwa ajili ya kuwabadilisha Kada, walibadilishwa na mishahara yao iliidhinishwa ipasavyo.

Ilisema upandishaji wa madaraja hutegemea mtumishi kuwa na sifa za kimuundo, uwapo wa ikama na bajeti ya mshahara kwa ajili watumishi waliopanda madaraja na muda wa kutumikia cheo kimoja kabla ya kupanda cheo kingine.

Vile vile, ilisema baadhi ya watumishi wanaojiendeleza kielimu hawapandishwi madaraja wala kuongezewa mshahara kutokana na kutozingatiwa kwa Mpango wa Mafunzo kwa Waajiri na Watumishi.

"Pia wengine wamekuwa wakijiendeleza katika fani tofauti na majukumu wanayotekeleza hususani wanaojiendeleza na kupata Shahada za Uzamili," ilisema.

Hata hivyo, ilisema watumishi wanaojiendeleza kielimu kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo wa Waajiri wao wanapandishwa madaraja au kubadilishwa Kada.

"Vilevile, Watumishi wanaojipatia sifa ya Stashahada ya Uzamili, Shahada ya Uzamili katika fani zao kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika miundo yao ya Utumishi wamekuwa wakipewa nyongeza mbili za mshahara," ilisema.

Ilieleza kuwa katika kuhakikisha kuwa watumishi wanapandishwa madaraja, serikali imetoa miongozo ya kuandaa Ikama na bajeti ya mshahara na waajiri husisitizwa kutenga bajeti hiyo kwa kuzingatia nafasi za ajira mpya, upandishaji vyeo, kubadilisha kada na uhamisho kwa mwaka husika wa fedha.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Kibaha Mjini (CCM), Slyvesty Koka, alihoji serikali haioni haja ya kuwaunganisha walimu wastaafu kuwa wanachama wa benki ya walimu ili iwasaidie.

Katika majibu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilisema hadi kufikia Februari, 2015 Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kiliwanunulia wanachama wake wote waliokuwa kwenye hati ya malipo ya serikali (pay roll), hisa zenye thamani ya Sh. milioni 50.

Ilisema thamani hiyo ni sawa na hisa 100 kwa kila mwanachama.

"Hisa nyingine za benki hiyo zinamilikiwa na kampuni tanzu ya Chama cha Walimu (Teachers Development Company - TDC) ambayo ina miliki asilimia tatu ya hisa kwa niaba ya walimu," ilisema.

Ilibainisha kuwa benki hiyo inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kibiashara na soko huria na inatoa fursa kwa waasisi ambao ni wanahisa kuendelea kunufaika na huduma na faida zinazotokana na benki hiyo.



# Vituo shikizi 182 vyasajiliwa shule za msingi

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema kwa mwaka 2019/20, imesajili vituo Shikizi 182 kuwa shule za msingi.

Hayo yalielezwa jana bungeni na wizara hiyo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Allan Kiula.

Katika swali lake, alisema jimbo lake limeanzisha shule shikizi ili kuwasaidia watoto wanaoanza madarasa ya awali na wale wa madarasa ya chini kutotembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

"Je, serikali ipo tayari kutambua juhudi hizo na kuzisajili shule hizo ikiwamo Iramba, Mnkola, Ilangida na Tanganyika,"alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema inatambua uwapo wa vituo shikizi na kwamba ni madarasa yanayoanzishwa chini ya shule mama katika maeneo yenye matatizo ya kijiografia na wanafunzi kushindwa kufika kwa urahisi shule mama.

"Wanafunzi wanaohusika na utaratibu huo ni wa elimu ya awali hadi darasa la III, madarasa hayo huhudumiwa na shule mama," ilisema.

Ilieleza kuwa serikali imekuwa ikiunga mkono juhudi za wananchi katika uanzishwaji na uendelezwaji wa vituo shikizi nchini ikiwamo wananchi wa jimbo hilo kwa kuvisajili vituo hivyo kuwa shule za msingi.

"Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesajili vituo shikizi 182 kuwa shule za msingi, kati ya hivyo, vituo viwili(Mgolombyo na Ndurumo) vipo jimbo hilo," ilisema.

Pia, ilisema vituo hivyo vitaendelea kusajiliwa ili kuwa shule za msingi iwapo vitakidhi vigezo vya usajili.

"Hadi sasa wizara haijapokea maombi ya usajili wa vituo shikizi vya Iramba, Mnkola, Ilangida na Tanganyika," ilisema.

Ilishauri Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na Wakurugenzi wengine wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wenye vituo shikizi kuwasiliana na Wadhibiti ubora wa shule katika maeneo yao ili vituo hivyo vikaguliwe.

Ilisema ukaguzi huo utaangalia kama vimekidhi vigezo vya kusajiliwa kuwa shule kamili kisha taarifa iwasilishwe wizarani kwa ajili ya usajili.



# Mbunge ahoji kusuasua miradi DMDP

MBUNGE wa Temeke (CCM), Abdallah Mtolea, amesema kumekuwa na kusuasua kwa ujenzi wa baadhi ya miradi iliyo chini ya Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alihoji ni lini miradi hiyo itakamilika kwa asilimia 100 na kama kuna mpango wa kuwapo kwa miradi ya DMDP awamu ya pili.

Katika majibu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilisema tangu mradi huo uanze kutekelezwa, jumla ya kilomita 187.59 za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. bilioni 357.26.

Ilisema katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi wa DMDP umeidhinishiwa Sh. bilioni 186.8 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kilomita 70 za barabara za lami na kazi nyingine zilizobaki.


Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 19, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


Ukurasa 14

**Wana-Serengeti waelimishwa nyumba kwa nyumba COVID -19**


Ukurasa 13

Corona ilivyokuja na gia ya kusambaratisha mtangamano


Ukurasa 12

**Elimu kuwa mwathirika wa kudumu wa corona**

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kiama madhara ya simu za mikononi uhai, mazingira- 2

MIAKA 47 iliyopita simu ya mkononi iligunduliwa, ilikuwa mwaka 1973, kazi iliyofanywa na timu ya wataalam wa kampuni ya Motorola wakiongozwa na Dk. Martin Cooper.

Leo matumizi ya simu hiyo yamebadili maisha kote duniani. Ni sawa na kusema ina umuhimu wa kipekee si kwa watu binafsi bali kwa taasisi na watu wote.

Matumizi ya simu hizo yamekuwa makubwa hasa kwa mataifa yanayoendelea pamoja na Tanzania, lakini ongezeko la simu linamaanisha uchafuzi mkubwa wa mazingira duniani na kitisho cha kuzagaa kwa sumu na kemikali zinazotokana na viambata (accessories) vilivyotengenezea simu hizo na betri zake kutokana na utupaji taka hizo. Wiki hii tunamalizia sehemu ya mwisho ya makala haya yanayoonya kuhusu kitisho cha simu za mikononi kwa afya. Endelea...



Mafundi simu mitaani ni wadau wanaohitaji elimu ili wafahamu njia bora wa kutupa simu na viambato vilivyochakaa. **PICHA: MTANDAO**

**MARADHI MAPAFUNI**

Simu ya mkononi pamoja na umuhimu wake imetengenezwa kwa sumu kali iliyo ndani ya madini ya 'beryllium'. Mitandao inayoainisha sumu inaieleza kuwa mara nyingi inakuwa katika hali mchanganyiko na metali ya shaba ikiitwa kitaalamu 'beryllium-copper alloy' ili kuongeza uimara na mnyumbuliko (flexibility).

Sumu hii inayotoka baada ya simu kutupwa ovyo na hivyo kuruhusiwa kusambaa inasababisha matatizo endapo mtu atakuwa karibu na vumbi la 'beryllium' na hivyo kusababisha maradhi yaitwayo 'beryllicosis' ambayo yanaweza kusababisha makovu ya kudumu kwenye mapafu na wakati mwingine kifo.

Kwa ujumla madhara ya betri na simu za mikononi kwa mazingira yanategemea aina ya betri na kwamba itatumika muda gani kabla haijaisha matumizi yake. Zile ambazo zinaweza kudumu muda mrefu na kuchajiwa zinaleta madhara madogo ukilinganisha na zinazodumu muda mfupi na zisizochajiwa.

Utupaji wa simu zilizochakaa na viambata vyake pamoja na athari za kikemikali kwa mazingira ni jambo linalotishia maisha.

Hii ni kwa sababu utupaji wa simu zilizochakaa mitaani hufanywa kiholela kwani zinatupwa ovyo kama taka nyingine hivyo zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa watu na mazingira.

Kemikali nyingi zilizomo kwenye simu za mkononi hujikusanya kama mafuta 'fats' kwenye mwili wa binadamu na wanyama pia.

Mitandao inauelezea mkusanyiko wa kemikali hizo kama 'persistent bioaccumulative toxins (PBTs)'.

Kemikali hizo au PBTs hujikusanya kwenye mafuta ndani ya miili ya watu na wanyama na sumu yake huongezeka taratibu kwa hivyo kuingilia mfumo mzima wa utegemezi wa ulaji 'the food chain' na kusababisha hatari zaidi.

Hivyo kuna haja ya kuchukua hatua na kurekebisha athari zake kabla hazijawa kubwa kama ambavyo inafikiriwa.

Taka hizi hatarishi ni suala linalogonga vichwa mataifa mengi ndiyo maana , mataifa yaliyoendelea yanatumia utaratibu wa kukusanya na kurejeleza betri hizo na simu zilizomaliza muda wake.

Si kwamba nchi zilizoendelea hazina changamoto hiyo ipo, ila utupaji wa simu katika nchi hizo mara nyingi zinasafirishwa kupelekwa katika mataifa maskini kama bidhaa za mitumba ili kuepukana na madhara yake japo biashara hiyo hufanywa kijanja.

Pamoja na hilo mataifa hayo yanahimiza matumizi ya betri zinazoweza kuchajiwa zaidi ambazo zinazoweza kudumu kwa muda mrefu ili kupunguza kasi ya kuharibu mazingira.

Vilevile katika nchi zilizoendelea kama vile mataifa ya Umoja wa Ulaya (EU), betri na simu zote zenye kemikali ambazo zimo kwenye orodha ya 'the Basel Convention's Annex I' zimezuiliwa kutumika tangu miaka 14 iliyopita yaani kuanzia Julai 1, 2006.

Hivi sasa EU imeweka udhibiti wa matumizi ya kemikali hizi hatarishi. Pia miongozo inatumiwa ya namna ya kuachana na matumizi ya betri zenye lead, cadmium, hexavalent chromium na simu zenye vizuio vya moto vyenye bromine, (brominated flame-retardants) kwenye vifaa vyote vya kielectroniki.

**UDHIBITI KWA TANZANIA**

Tanzania inahitaji kuwa na sheria na miongozo ya namna ya kutupa taka zitokanazo na vifaa vya kielektroniki na pia itumie sheria za kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kama vile mkataba wa Basel (the Basel Convention) ili kuelekeza namna ya kudhibiti utupaji ovyo wa simu za mkononi na betri zake.

Aidha, mamlaka zinawajibika kudhibiti kuingiza simu na vifaa vya kieletroniki vya mitumba kwa vile vinaharibika kwa muda mfupi na kuleta madhara mapema.

Ni vyema serikali na mamlaka za kuhifadhi mazingira kwenye mikoa na wilaya, miji na majiji zikaweka vituo maalum vya kukusanya na kutupa simu na vifaa vingine vya kieletroniki vya mitumba ili kudhibiti uharibifu mkubwa wa mazingira unaoweza kuletwa na utupaji holela uliopo sasa.

Aidha, ni vyema kuangalia uwezekano wa kufanya urejelezaji 'recycling' ya baadhi ya vifaa vinavyotumika kutengeneza simu. Pia serikali idhibiti uingizaji wa simu za bei duni na kuhakikisha kuwa bei za simu hazitofautiani ili kuepusha kuwa na simu nyingi bila sababu.

Kupunguza idadi ya wingi wa simu na viambata vya kutupwa zinapomaliza muda wa matumizi kutasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Utaratibu ukitumika vijijini ambako kuna watumiaji wengi wa simu na idadi kubwa ya simu za mitumba utasaidia kupunguza uchafu wa mazingira na kitisho kwa binadamu.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA



Msongamano kupindukia vyuoni pamoja na darasani ni changamoto inayoifanya elimu kuwa mwathirika namba moja wa corona. **PICHA: MTANDAO**

# Elimu kuwa mwathirika wa kudumu wa corona

WAKATI nchi za Magharibi zinachukua hatua ya kurejea kwenye taratibu za awali kuwezesha watu kuanza kuishi kawaida katika mazingira tofauti, shinikizo la Tanzania kufuata kanuni za nchi hizo za kufungia watu ndani bado lipo, ingawa serikali haiitilii maanani kama wapinzani wake wanavyotaka.

Kingine kinachoonekana katika nchi za Magharibi ni kuangalia kwa kiwango gani hali za maisha zitaweza kurudi kama kawaida, au ni kwa kiwango gani 'new normal,' au kawaida mpya itabakiza nchi hizo katika mkwamo wa shughuli tofauti.

Wanaoingia katika soko la ajira wakiwa na vyeti wanaweza kuwa waathiriwa wakubwa zaidi wa mkwamo huo, ajira zikibaniwa zaidi.

Kwa hapa nchini kuna eneo moja ambalo serikali imeahidi kutoa ajira kwa wingi zaidi, ambalo ni fani ya udaktari na uuguzi, kwani kuna kila dalili kuwa gonjwa la corona litaendelea kuwapo kwa siku nyingi.

Magonjwa ya aina hiyo yaliyopita kama SARS na MERS (yote mawili yanaathiri njia za hewa mapafu na pua 'respiratory syndrome'. Tatizo la kupumua, moja la kimataifa likianzia China mwaka 2012 na jingine lilijikita tu Mashariki ya Kati hasa kuanzia 2014 hata sasa bado yapo.

> Ndiyo hapo unakuta kuna haja ya mkakati wa ajabu ambao hadi sasa haujafikiriwa, jinsi ya kunasua sekta ya elimu na elimu yenyewe katika maisha ya watu.

Hata Ukimwi bado hauna chanjo licha ya kuwa umekuwapo kuanzia mwaka 1981 ambako vifo vilianza hasa Marekani.

Sekta ya elimu inaweza kuwa mwathirika wa kudumu wa gonjwa la corona kwa sababu almradi ugonjwa upo shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii hazitarudia hali yake ya kawaida.

Elimu ina lengo kubwa katika maisha la kumwezesha mtu apambane na mazingira aweze kujipachika katika sekta moja au nyingine afikie viwango vya vipaji vyake kimapato na kisaikolojia, ndiyo mtu anaweza kujisikia vizuri. Kupata elimu na kushindwa kuitumia katika fani husika ni hasara.

Kuathirika kwa elimu katika kipindi cha awali ni kufungwa shule na vyuo kwa muda usiojulikana, na katika nchi za Magharibi wanajaribu kutatua suala hilo kwa njia tofauti za majaribio.

Ziko nchi zimeanza na shule za sekondari kwani zinaona vijana hao wana uwezo zaidi wa kufuata maelekezo ya afya, lakini wengine wameanza na shule za msingi na hata chekechea kwa hisia kuwa siyo rahisi wao kuambukizana gonjwa la corona. Ni hapa na pale tu wanafikiria habari za kufungua vyuo vikuu, kwani mazingira yao ya maisha hufanana na ya mtaani.

Wanaofuatia tatizo la ajira baada ya kuhitimu wanajua kuwa lilishaanza kuota mizizi kwa takriban miongo miwili ambako vijana wanamaliza elimu ya chuo kikuu na hawana pa kwenda kwenye uhakika wa ajira.

Kwa miaka mingi vijana wamekuwa wakiambiwa waangalie njia za 'kujiajiri,' ambayo kisaikolojia ni kama kejeli. Yaani mtu asiye na ajira kufumba na kufumbua anakuwa mwekezaji, anaweka mtaji na kuangalia biashara atakayofanya, aanze kutafuta mwajiriwa na wa kwanza awe yeye mwenyewe! Ni urasimu kupuuzia tofauti ya ajira, uwekezaji.

Mradi mizunguko ya watu ya kawaida itakuwa imepungua, na siyo rahisi kuona itarudia vipi hali ya kawaida wakati kuna hatari ya maambukizo watu wakikaa makundi makubwa kwa muda wowote ule, shughuli za kiuchumi na kijamiii hazitatengemaa?

Ni kupungua kwa dhati kwa mahitaji ya kawaida ya bidhaa na huduma za kijamii. Na katika mazingira ambako kusinyaa kwa ajira tayari kulishaota mizizi, halafu jitihada zinaendelea vijana wasome kwa hali yoyote ile mitandao au shule kufunguliwa hatimaye na kusoma kawaida ajira zilizobakia zitasinyaa pia.

Ndiyo hapo unakuta kuna haja ya mkakati wa ajabu ambao hadi sasa haujafikiriwa, jinsi ya kunasua sekta ya elimu na elimu yenyewe katika maisha ya watu.

Hitaji hilo linaendana na lile la ajira kutengemaa angalau kurudi katika hali iliyokuwepo awali, licha ya kwamba ilikuwa na mapengo hayahesabiki ya kuoanisha matarajio katika maisha na kupitia ngazi hii au ile ya elimu. Inafikia mahali ambapo ajira zinapatikana kwa baadhi ya watu kufariki au kustaafu, na siyo kila anayestaafu anahitajika mbadala, wengi wanaofariki walikuwa tayari hawako tena katika ajira.

Tuseme ndiyo janga ambalo dunia imefikia hivi sasa,kuwa walio na umri mkubwa ndiyo walio hatarini zaidi na janga la corona, na kwa vile corona imepunguza kwa kiasi kikubwa shughuli za kila siku zinazohitaji huduma na zinazalisha bidhaa, ni katika zile chache zilizobali ushindani utabaki.

Ndiyo hapa linaingia janga la kungoja corona ipunguze watu katika maeneo tofauti halafu wengine waingie kazini, endapo corona itagusa walio katika umri wa kufanya kazi. Hata hivyo kimsingi matarajio hayo ni kwa wale walio katika sekta ya umma, binafsi huweza kupuuza kuwa kuna nafasi nyingine imepatikana, kwani kwa sasa wanatafuta njia kupunguza watu zaidi.

Watu wanapunguzwa katika ajira kwa mwanya wowote ule kwani huduma zao hazihitajiki kwa vile matazamio ya kawaida ya kupanua shughuli za kampuni aina yoyote ile sasa zimedumaa.

Na hata zile za mazishi zinauza majeneza na kukodisha magari ya kupeleka, siyo huduma kwa watu wengi wanaohudhuria mazishi kwani hiyo hairuhusiwi wakati wa janga la corona.

Corona ni mahali ambapo watu wanalazimishwa kupiga 'mark time,' kusimama walipo, hata kama serikali inaruhusu 'kuchapa kazi kujenga taifa' mlolongo wa vizuizi vya nje ya nchi na hata ndani ya nchi vinadumaza shughuli za uchumi.

Hali hii ikiendelea kila mtu atakuwa anaishi kwa aina moja au nyingine ya nguvukazi isiyo na uhusiano wa moja kwa moja na elimu. Siyo rahisi kufafanua 'mustakabali' wa elimu katika mazingira hayo, kusoma mtandaoni, pasipo na ajira.

ELIMU

## NA MASHAKA MGETA

# Corona ilivyokuja na gia ya kusambaratisha mtangamano



Viongozi wa Afrika katika moja ya shughuli za mikutano ya kudumisha mtangamano. Wakuu hawa wanatakiwa kushirikiana katika kukabili corona badala ya kusambaratika. **PICHA: MTANDAO**

JANGA la maambukizo ya ugonjwa wa COVID -19 limeendelea kuathiri sehemu kubwa ya mataifa duniani, huku kila nchi ikijikita kuvidhibiti virusi hivyo, kwa kutumia mbinu, rasilimali na desturi zake.

Maambukizo hayo yaliyoanzia kwenye mji wa Wuhan jimbo la Hubei nchini China, yameharibu mifumo ya maisha ya watu katika nyanja tofauti zikiwamo za kisiasa, kiuchumi, michezo, imani na dini.

Kwa mfano, nchini Ethiopia, uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Agosti mwaka huu, uliahirishwa kutokana na athari zilizochangiwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Bodi ya Taifa ya Uchaguzi nchini humo (NEBE) ilitangaza kuahirisha uchaguzi huo wa rais na wabunge ambao ungekuwa kipimo kwa serikali ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed, baada ya mashauriano na vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi huo. Hivyo, jambo kubwa lililopo sasa kwenye mataifa mengi (kama si yote duniani) ni kuvidhibiti virusi vya corona kupitia njia zinazowezesha upatikanaji wa tiba, wakati watu wakiendelea kujikinga dhidi ya maambukizo.

Bara la Afrika lenye jumla ya nchi 55 halikukwepa kupata na kuthibitisha maambukizo ya virusi vya corona yalitokea nchini China, ama katika nchi nyingine ambazo raia ama wageni wake waliingia kutoka mataifa yaliyoathirika, na wao wakiwa miongoni mwa wenye virusi hivyo.

Ndivyo ilivyokuwa pia kwa Tanzania ambayo Machi 16, mwaka huu, ilitangaza rasmi kuwa na mgonjwa wa kwanza wa COVID - 19, Isabella Mwampamba, mkazi wa jijini Arusha.

Ukweli ni kwamba, kutokana na asili ya kuenea kwake, maambukizo ya virusi vya corona hayakwepi umuhimu wa ushirikiano kuanzia ngazi ya familia, nchi, jumuiya za kikanda na kimataifa.

> “Hali hiyo ni tofauti na ilivyo kwenye mpaka wa Kasumbalesa unaozitenganisha Zambia na DRC ambapo inajulikana kwa muda wa madereva kuwapo hapo kwa sababu za kutimiza vigezo kuwa ni siku mbili.

Lakini mikakati ya ‘mamlaka’ moja inaweza kutofautiana na ile inayotumiwa na ‘mamlaka’ nyingine, kama ilivyo kwa matumizi ya rasilimali zake, lakini lengo kuu likabaki kuwa ni kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona.

Hivi karibuni, kumeibuka malumbano hasa kwa mataifa ya Afrika kuhusu namna bora ya ushirikiano barani humo na pia kwenye jumuiya za kikanda ikiwemo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hali inayoweza kufifisha udhibiti wa maambukizo ya virusi hivyo. Kama inavyoeleweka kwa wengi, mataifa ya Afrika yanatofautiana kwa namna nyingi, kama ilivyo kwa nchi za mabara mengine. Miongoni mwa tofauti hizo ni idadi ya watu na uwezo wa kiuchumi na rasilimali kwa nchi husika.

Ndiyo maana linapokuja suala kama la kuwafungia watu wasitoke nje ikiwa ni moja ya mbinu za kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona, nchi hizo zimetekeleza kwa namna tofauti, huku nyingine zikishindwa kufikia hatua hiyo kutokana na sababu zinazowapa nguvu ya kufanya hivyo.

Mtaalamu wa masuala ya ushirikiano wa kimataifa asiyetaka kutajwa gazetini kutokana na nafasi yake katika utumishi wa umma, anasema tofauti za kimitazamo na mikakati ya mataifa ya Afrika havipaswi kuwa sababu ya kuvuruga uhusiano uliodumu kwa miaka mingi sasa.

Anatoa mfano kuwa hata nchi za Ulaya na Marekani waliopo kwenye mazungumzo ya uboreshaji wa uhusiano wa kibiashara, lakini wakikabiliwa na changamoto kadhaa zinazotokana na maambukizo ya virusi vya corona, bado wana ‘makandokando’ yanayoathiri azma nia, lakini wanavumiliana ili kufikia lengo hilo.

Johnson Mwikabe, mtafiti katika masuala ya diplomasia ya uchumi anasema zipo taarifa nyingi zilizotolewa na viongozi wa mataifa ya Afrika, na hatua kadhaa zinazolenga kudhibiti kasi ya maambukizo hayo, akitoa mfano wa kufungwa kwa mpaka wa Nakonde unaozitenganisha Tanzania na Zambia.

Mtandao wa Lusaka Times ulimkariri Waziri wa Afya wa Zambia, Dk Chitalu Chilufya, aksema Rais Edgar Lungu, wa nchi hiyo aliagiza kufungwa kwa muda mpaka wake kuanzia Mei 11, mwaka huu, ili kutoa fursa kwa utekelezwaji wa mikakati mipya ya kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona.

Kwa upande wa Tanzania, Rais John Magufuli, alishasisitiza msimamo wake wa kutofunga mipaka ya nchi akisema kuna nchi ambazo hazina bandari zinazotegemea mizigo yao kupita kutokea bandari ya Dar es Salaam.

Wakati Zambia ikichukua hatua hiyo itifaki ya nchi za SADC katika kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona inaonyesha kila nchi inaruhusiwa kudhibiti maambukizo hayo kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa na hali halisi ya nchi husika huku usafirishaji wa bidhaa muhimu ukitakiwa kuzingatiwa kwa nchi wananchama.Ni kutokana na hali hiyo, madereva kadhaa wa Tanzania waliokwama mpakani hao baada ya hatua iliyofikiwa na Zambia, wameelezea kusitikishwa kwao na kwamba wanapata usumbufu na matumizi makubwa ya fedha yaliyo nje ya bajeti zao.

Taarifa za ndani ya Zambia zinadai kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia kasi ya kuenea kwa maambukizo ya corona kwenye eneo hilo la mpaka ni vitendo vya ngono vikiwahusisha zaidi madereva wa malori na wanawake wanaofanya biashara ya ngono.

Miongoni mwa madereva hao, Kaijage Method kutokea jijini Dar es Salaam anakaririwa na BBC, hivi karibuni akisema kuwa, walipata taarifa hizo baada ya kukutana na wakala wa uvushaji magari mpakani hapo.

Kwa mujibu wa Kaijage, wakala huyo aliwajulisha kuhusu kuzuiliwa kwa magari kulikotokana na kufungwa kwa mpaka huo na kwamba idadi ya malori yaliyokuwa yakiwasili mpakani hapo kuingia Zambia ama kupita nchini humo kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ilikuwa inaongezeka.

Anasema hali hiyo ni tofauti na ilivyo kwenye mpaka wa Kasumbalesa unaozitenganisha Zambia na DRC ambapo inajulikana kwa muda wa madereva kuwapo hapo kwa sababu za kutimiza vigezo kuwa ni siku mbili.

Mbali na hali iliyopo Zambia, wapo viongozi na wanasiasa wa mataifa wengine kama Rais Yoweri Museveni wa Uganda, Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini na kinara upinzani, Raila Odinga, waliokaririwa kutoa matamko yenye viashiria vya ‘hali kutokuwa nzuri’ kwa ushirikiano wa kikanda katika kuikabili corona.

Mathalani, Rais Ramaphosa aliitisha kikao cha viongozi wa ‘nchi jirani wa Afrika Kusini’ na kusema kilifanyika baada ya kuwasiliana na Mwenyekiti wa SADC, Rais Magufuli, akataka washiriki watume hoja zao kwa njia ya maandishi.

Lakini Katibu Mtendaji wa SADC, Dk Stergomena Lawrence Tax, anasema Rais Magufuli hakupaswa kuhusishwa moja kwa moja na mkutano ulioitishwa na Rais Ramaphosa kwa vile haukuwa ‘umebeba’ ajenda ya jumuiya hiyo.

“Huo ulikuwa mkutano wake binafsi Ramaphosa aliouitisha na kuwashirikisha viongozi wa nchi zilizo jirani na Afrika Kusini,” anasema Dk Tax.

***Maoni: 0754691540***

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Wana-Serengeti waelimishwa nyumba kwa nyumba COVID -19



Wananchi wakiwa kwenye kikao kuelimishwa kuhusu mbinu za kujikinga na virusi vya corona: **PICHA ZOTE NA MPIGA PICHA WETU**



Mtumishi wa afya Serengeti, akitoa elimu kuhusu kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona. **PICHA: MTANDAO**

MOJA ya mambo muhimu ambayo serikali inahimiza kipindi hiki cha tishio la maambukizo ya virusi vya corona, ni utoaji wa elimu katika jamii ili izingatie mbinu sahihi za kujikinga na kuwa salama zaidi wakati huu ambao corona inaendelea kuitesa dunia.

Serikali inaamini kwamba iwapo kila Mtanzania atafikiwa na elimu hiyo na kuizingatia, itakuwa rahisi kufahamu njia za kujikinga na ugonjwa huo.

Elimu inayotakiwa kuzingatiwa, ni jamii kunawa mikono kwa sabuni, kutumia vitakasa mikono kila mara na pia kila mtu kuvaa barakoa akiwa nyumbani na hata anapotoka kwenda kwenye shughuli zake za kila siku.

Kwa ujumla hiyo ndiyo elimu ya wataalamu wa afya ambayo kila Mtanzania anatakiwa kuizingatia, lengo likiwa ni kujilinda dhidi ya virusi vya corona ambavyo bado havina tiba.

Kamati ya Kupambana na Virusi vya Corona ya Wilaya ya Serengeti mkoani Mara imelizingatia hilo na sasa inashirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo kuepusha wananchi na maambukizo ya ugonjwa huo.

> Elimu hii inatakiwa kutolewa kwa wingi, kwani jamii na hasa za vijijini bado ni kama hazijaelewa tatizo hili ambalo limeikumba dunia, kwani mikusanyiko ipo kama kawaida.

Kamati hiyo ambayo iko chini ya ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo, Nurdin Babu, imekuwa ikizunguka katika vijiji mbalimbali kuelimisha jamii ili izingatie maelekezo ya wataalamu wa afya.

Babu anasema, kamati hiyo inashirikiana na wadau wengine wakiwamo nyumba salama ya mjini Mugumu katika kutoa elimu kwa jamii katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

"Kuna umuhimu wa kutelekeza ushauri wa wizara ya afya kwa vitendo, ndiyo maana kuna kamati hiyo. ambayo inazunguka kuelimisha umma, lakini ikifuata tahadhari zote hasa kuepuka msongamano," anasema Babu.

Mkuu huyo wa wilaya anasema, tangu kuingia kwa ugonjwa huo nchini, kumekuwapo na sintofahamu, kutokana na baadhi ya watu kupotosha umma, hivyo ni muhimu jamii ipate elimu sahihi.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi isiyo ya kiserikali ya Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly, ambaye taasisi yake inashiriki katika kutoa elimu, anasema jamii inatakiwa kubadilika.

"Elimu hii inatakiwa kutolewa kwa wingi, kwani jamii na hasa za vijijini bado ni kama hazijaelewa tatizo hili ambalo limeikumba dunia, kwani mikusanyiko ipo kama kawaida," anasema Rhobi.

Rhobi anasema, serikali inajitahidi kuelimisha umma, lakini jamii nayo inatakiwa kubadilika, kwa vile baadhi ya watu hawajawa makini katika kujikinga na ugonjwa huo.

"Lakini pia kuna tatizo la umaskini kwani baadhi ya watu wanashindwa kununua barakoa, hayo na mengine mengi ambayo tunayashuhudia vijijini, yanaonyesha kuwa bado elimu zaidi inahitajika," anasema.

### KULINDA WASICHANA

Mkurugenzi Rhobi huyu anasema, taasisi yake inalea wasichana wanaokimbia ukeketaji kutoka nyumbani kwao, na kwamba wameamua kuwaweka katika mazingira ambayo hawawezi kuambukizwa na ugonjwa huo.

Anasema, kila mara taasisi yake inapokea wasichana wanaokimbia vitendo vya ukeketaji, hivyo ni muhimu kuhakikisha wote wanakuwa salama wapya na hata waliopo nyumba salama.

"Kwanza wamepewa elimu ya kujikinga na corona na wanavaa barakoa, ambazo wanashona wenyewe na nyingine tunazigawa na kaya maskini na pia zipo ambazo wanaziuza," anasema.

Aidha, anasema, wasichana wapya wanaookolewa katika vitendo vya ukeketaji, wanawekwa katika chumba maalum kwa siku 14 wakifanyiwa vipimo kabla ya kuunganishwa na wenzao.

Rhobi anasema, lengo ni kuhakikisha usalama wao, na kwamba elimu inaendelea kutolewa kila mara ikiwamo kuwazuia walimu wanaoishi nje ya kituo cha nyumba salama hadi hapo hali itakapotulia.


"Walimu wanaoishi nyumba salama, hao wanaendelea na kazi kama kawaida, kwa sababu wamefanyiwa vipimo na kuhakikisha wako vizuri, hivyo wanaendelea kuwahudumia wasichana kama kawaida," anasema.

Anafafanua kuwa masomo ya ufundi yanaendelea kutolewa kama kawaida, lakini kwa tahadhari na pia wasichana wamekuwa wakijifunza somo la Kiingereza kila Alhamisi kupitia video kutoka Uingereza.

Anasema, kuna mwalimu wa kujitolea kutoka nchini humo, ambaye amekuwa akiwafundisha somo hilo, kama njia ya kuwaandaa vizuri kwa lugha hiyo wasichana hao walio nyumba salama ya Mugumu.

Anasema, nyumba salama ya Mugumu ina wafadhili mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ambao wameiwezesha taasisi hiyo kujulikana hadi kutambuliwa na kupata ushirikiano na serikali.

"Tunashukuru ushirikiano ambao tunaupata kwa serikali nasi tupo mstari wa mbele katika vita hii ya kupambana na corona, ndiyo maana tunazunguka na kamati kutoa elimu kwa jamii," anasema Rhobi.





# Waziri aagiza kushughulikiwa haraka mashauri ya walimu 110

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (TSC) kushughulikia mashauri 110 ya walimu ili kutolewa uamuzi haraka.

Jafo alitoa agizo jana jijini hapa baada ya kuwaapisha mwenyekiti na wajumbe nane wa tume hiyo walioteuliwa hivi karibuni.

Alisema mashauri hayo yalikuwa yanasubiri wajumbe hao ili yatolewe maamuzi na kuweka mambo sawa hivyo baada ya kuapishwa waanze kazi hiyo ndani ya wiki hii.

"Hizi rufani 110 za walimu mkazishughulikie haraka muanze hii kazi ndani ya wiki hii, ili mambo yawe sawa, uchaguzi wenu sio wa kubahatisha nina imani tume itafanya kazi iliyokusudiwa," alisema.

Akizungumzia suala la nidhamu, Jafo aliitaka tume hiyo kutolala katika kusimamia nidhamu ili isishuke.

"Mkaangalie kuna walimu ambao kazi yao ni kutoa notisi ubaoni na wanafunzi wa shule za serikali wananakiri badala ya kufundisha wakati wanalipwa mshahara, lakini wanaenda kufundisha wanafunzi wa shule za binafsi," alisema.

Alisisitiza kuwa tume hiyo kufanya kazi kwa weledi na kushughulikia malalamiko ya walimu.

"Tamisemi inasimamia watumishi wa umma zaidi ya asilimia 70 na asilimia 50 ni walimu. Tume ina kazi kubwa ya kusimamia nendeni mkatimize majukumu yenu ipasavyo," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Tume, Prof. Willy Komba, alimhakikishia waziri kuwa tume yake itafanya kazi kwa weledi, juhudi, maàrifa katika kuwatumikia wadau wao ambao ni walimu ili wapate huduma wanayoitarajia.

"Tunahitaji sana ushirikiano ili tuweze kutukeleza majukumu yetu. Na tuko tayari kuanza kufanyakazi kuanzia sasa."

# 280,000 wachangamkia uanachama CHF

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

ZAIDI ya wanachama 280,000 Mkoa wa Dodoma, wamejiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) ambao huduma zake zimeboreshwa zaidi tofauti na ilivyokuwa awali.

Awali, mgonjwa alikuwa akitibiwa katika mkoa wake alipo, lakini hivi sasa mgonjwa anaweza kutibiwa mahali popote atakapokuwa kwa kadi yake ambayo amelipia gharama ni Sh. 30,000.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa CHF mkoani humo, Dk. Francis Lutalala, alisema huduma za mfuko huo zimeboreshwa ndio sababu wanachama wameongezeka.

Alisema mkoa bado unaendelea kuwashawishi wanachama hususani waliopo vijijini ili wajiunge na mfuko huo ikizingatiwa msimu wa mavuno umefika, hivyo wakazi wa maeneo mbalimbali watakuwa na uwezo wa kujiunga na mfuko huo.

Hata hivyo, alisema CHF imeshalipa fedha katika hospitali mbalimbali ili wateja wake wasipate shida pale wanapokwenda kupata matibabu kwenye vituo vya afya hadi hospitali za mkoa.

Alisema lengo lao ni kuona kila Mtanzania anakuwa na bima ya afya ambayo ni muhimu kila mmoja kuwa nayo ili kuwa na uhakika wa matibabu.

"Tumefanya kampeni wilayani Mpwapwa, Chamwino na tunatarajia kwenda wilaya zingine kutoa elimu ya nini maana ya mtu kuwa na bima ya afya iliyoboreshwa," alisema.

Dk. Lutalala alisema hivi sasa mtu akiwa na CHF kila mahali anatibiwa tofauti na ilivyokuwa awali, ambapo alikuwa anapata matibabu katika mkoa ambao amekata bima hiyo.

Alisema wamepanga kutumia msimu wa mavuno kwenda maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwashawishi wananchi kujiunga na mfuko huo.

Mratibu huyo alisema wanachama waliopo bado idadi haitoshi hivyo wanahitaji kuongeza wengine ili kufikia malengo waliyojiwekea.

**Tumefanya kampeni wilayani Mpwapwa, Chamwino na tunatarajia kwenda wilaya zingine kutoa elimu ya nini maana ya mtu kuwa na bima ya afya iliyoboreshwa**



Mkulima Yohana Mwalimu, akianika uwele katika Kijiji cha Hombolo, mkoani Dodoma juzi. Kuisha kwa msimu wa mvua kumetoa nafasi kwa wakulima kuanza kukausha mazao yao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu ashtukia ufungaji mipaka hofu ya corona

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la Free Pentecostal of Tanzania (FPCT), Jimbo la Dodoma, Timoth Mathayo, amesema mapambano dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona hayawezi kufanikiwa kwa kufunga mipaka ya nchi.

Badala yake wameshauriwa kuendelea kuomba Mungu ili awaepushe na maambukizo ya ugonjwa huo.

Akizungumza na waumini wa Kanisa hilo Mtaa wa Chamwino juzi, Askofu Mathayo alisema ugonjwa unaotokana na virusi haujulikani utatoweka lini, hivyo si busara kuwazuia watu wasifanye shughuli zao za kujiingizia kipato kwa kufunga mipaka.

Alisema kuwa ugonjwa huo ni ugonjwa ambao unaambukizwa kwa hewa, maji maji na kugusana, hivyo kinachoweza kuuondoa ni nguvu ya Mungu pamoja na kutimiza masharti ya wataalamu wa afya.

Alisema kuwa kufunga mipaka hakuwezi kusaidia bali kinachotakiwa ni kumwomba Mungu aondoe janga hilo, huku watu wakiendelea kuhamasishwa kuzingatia masharti ya kujihadhari ya maambukizo ya virusi hivyo.

"Nataka kuwaambia washirika wangu pamoja na Watanzania kwa ujumla kuwa ugonjwa wa corona ni ugonjwa kama magonjwa mengine... gonjwa hili haliwezi kuzuiliwa kwa bunduki wala risasi, kinachoweza kuondoa janga hili ni kumuomba Mungu sambamba na kufuata masharti yanayotolewa na wataalamu wa afya," alisema.

Aliongeza: "Ninachosema ni hivi corona kamwe haiwezi kuthibitiwa kwa kufunga mipaka au kuwafungia watu ndani," alisema na kuongeza:

"Zaidi watawasababishia wananchi kuwa na hali ngumu ya kimaisha tofauti kama wangepewa uhuru wakufanya shughuli zao."

Aliwaasa Watanzania kuachana na tabia ya kuwa na hofu pale wanaposikia idadi ya vifo kuongezeka katika mataifa ya Ulaya, na kuwataka kuendelea kuomba Mungu zaidi pamoja na kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo.

"Binafsi niseme kuwa nimekuwa mwanafunzi wa Rais John Magufuli kwa kufuata maagizo yake ya kutoteteleka wala kuwajaza watu hofu juu ya ugonjwa huu... ninachofurahia ni kutokana na imani yake kubwa kwa Mungu aliyonayo ya kuamini kuwa maombi ndiyo njia pekee ya kumaliza virusi ya ugonjwa wa corona," alisema.

HABARI MBEYA

# Taasisi ya Tulia yamwagia kaya 80 sadaka ya futari

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TAASISI ya Tulia Trust Fund, inayosimamiwa na Naibu Spika wa Bunge wa Tanzania, Dk. Tulia Akson, imekabidhi msaada wa mahitaji ya futari kwa kaya 80 kama sehemu ya sadaka kwa ajili ya Waislamu kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akikabidhi msaada huo kwenye Msikiti wa Forest ya zamani, Meneja wa Taasisi hiyo, Jacqueline Boaz, alisema lengo ni kuhakikisha makundi mbalimbali yenye uhitaji ndani ya jamii hususani ya Kiislam kipindi hiki wanapata chakula ili nao wafuturu.

Alisema huu ni mwaka wa tatu mfululizo wanatoa futari ili iwasaidie makundi maalum mfungo wa Ramadhan ili wajione sehemu ya jamii inayotambuliwa.

"Dhamira yetu ni kuwafikia watu wengi lakini kwa sababu ya masuala ya bajeti kuna utaratibu tunaufanya kwa sasa tumewafikia wenye uhitaji wakiwamo wazee, walemavu na kaya maskini ili nao wafuturu chakula kizuri," alisema Boaz.

Msaada wa futari uliotolewa ni pamoja na mafuta lita tano, mchele kilo tano, sukari kilo tano na unga kilo tano ambapo kila kaya yenye uhitaji ilipatiwa.

Akipokea msaada huo, Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), Mkoa wa Mbeya, Mtawa Kapalata, mbali ya kuipongeza Taasisi ya Tulia Trust kutoa msaada huo, alisema taasisi hiyo imekuwa kiungo katika jamii kwa kutoa misaada bila kujali itikadi za kidini na vyama.

Alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka hasa kwa familia maskini ambazo hazina uwezo wa kumudu gharama za kununua mahitaji ili kufuturu kutokana na hali ya uchumi.

Mjumbe wa Umoja wa Maimamu jijini Mbeya, Ibrahimu Bombo, alisema waumini waendelee kumwomba Naibu Spika wa Bunge la Tanzania Dk. Tulia Ackson na serikali kwa sababu ya mambo ya maendeleo anayoyafanya katika jamii.



Mjumbe wa Umoja wa Maimamu Jiji la Mbeya, Ibrahimu Bombo (kushoto) na Katibu wa Baraza Kuu la Waislam (Bakwata), mkoani humo, Mtawa Kapalata (wa pili kushoto), wakipokea msaada wa vyakula, kutoka kwa Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz, vilivyotolewa na taasisi hiyo zawadi ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa ajili ya kaya 80, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mtafiti awapa mbimu wakulima wa ndizi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MTAFITI wa mboga na matunda kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari), Kituo cha Uyole, Daud Mbongo, amewashauri wakulima wa ndizi kutoa taarifa kwa wataalamu wanapobaini ugonjwa wowote katika zao hilo ili kuongeza tija na uzalishaji.

Mbongo alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na baadhi ya wakulima wa Kata ya Kisondolea katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Alisema zao hilo ambalo hutegemewa kwa asilimia 30 na Watanzania kama chakula na tunda, linahitaji uangalizi wa hali ya juu ikiwamo tiba ili mmea wake uweze kustawi.

Mbongo alisema kumekuwa na tatizo kwenye kuhudumia mmea wa mgomba kutokana na wakulima wengi kutokuwa na uelewa pamoja na kukabiliana na minyoo shambani.

"Migomba huathirika sana na visumbufu vya mimea kama magonjwa, bungua wa migomba, minyoo ya mizizi na hata ngedere ambao hula ndizi zinapoivia shambani... hivyo wakulima wanapaswa kuwatumia zaidi wataalamu ili kukabiliana na minyoo pamoja na magonjwa mengine ili wasipate hasara," alisema Mbongo.

Aliongeza kuwa minyoo ni viumbe ambao hawaonekani kwa macho, bali huonekana kwa kutumia lensi, na kwamba makazi yake huwa kwenye udongo na hushambulia mizizi ya mazao kama migomba na mingineyo.

Alisema minyoo hushambulia mizizi ya migomba na kuisababisha ishindwe kuchukua maji na virutubisho kutoka kwenye udongo, hivyo migomba kudhoofu hatimaye hutoa mazao hafifu au kunyauka kabisa.

"Kuna minyoo ya aina nyingi, baadhi ya minyoo ni kama minyoo fundo (root knot nematodes) aina hii ya minyoo hutengeneza mafundo kwenye mizizi ya mmea kiasi kwamba yanaweza kuonekana kama shanga, minyoo michirizi (lesion nematodes) aina hii ya minyoo inapoingia kwenye mizizi huachia michirizi ya kahawia au myekundu na mwisho michirizi huishia kwenye uozo mweusi.

"Alisema aina ya minyoo inayochimba (burrowing nematodes), hupenya na kuingia ndani ya mizizi ya mimea na kula kwa kutengeneza mashimo," alieleza Mbongo.

Mbongo aliwaelekeza wakulima hao kuwa kuna njia mbalimbali za kukabiliana na minyoo ya mizizi ikiwamo kusafisha shamba la migomba muda wote, kutochukua vipando kutoka kwenye shamba lililo na ika na minyoo ya mizizi.

Mkurugenzi wa Kituo cha utafiti cha Uyole Tari, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliwaambia wakulima kuwa kituo hicho kinabuni teknolojia mbalimbali za kilimo ili zitumike kuboresha kipato cha chao, na kwamba waendelee kutembelea ili kupata elimu ya kilimo bora.

# Madiwani Chunya waiangukia TRA kodi ya majengo

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Chunya, wameomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kutoa elimu kwa wananchi juu ya ulipaji kodi ya majengo ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato katika wilaya hiyo.

Madiwani waliyaeleza hayo mwishoni mwa wiki, baada ya kubaini vikwazo vya ukusanyaji kodi za majengo kwa baadhi ya wananchi kutokana na kutokuwa na uelewa wa aina gani ya nyumba inayotakiwa kulipiwa.

Miongoni mwa madiwani hao, Alex Kinyamagoha wa Itewe alisema suala la kulipa kodi ni la kisheria hivyo kila mwananchi anapaswa kufanya hivyo, lakini kinachotakiwa ni kuwaelimisha kwanza kwa sababu bado hawana uelewa wa kutosha juu ya namna gani wanalipa na ni nyumba zipi ninazotakiwa kulipiwa.

"Sio kwamba wananchi hawataki kulipia kodi za majengo bali hawana elimu ya kutosha ni jambo geni kwao, tuendelee kuwafundisha taratibu wataelewa," alisema Kinyamagoha.

Ofisa wa TRA, wilayani humo, Osmund Mbilinyi, alikiri kuwa mwitikio wa wakazi wa wilaya hiyo, katika ulipaji kodi ya majengo ni bado ni mdogo.

Alisema hadi sasa hafahamu sababu inayosababisha wasijitokeze kulipa kodi kwamba ni hali ya uchumi au kwa kuwa ni suala geni kwao.

Aliongeza kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa kuwatumia viongozi ngazi ya kijiji na kata sambamba na kuandaa mikutano ya hadhara ili kuongeza ushawishi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, aliwataka maofisa wa TRA kushirikiana kwa karibu na ofisi yake pamoja na mkurugenzi ili kuhakikisha wanatatua tatizo hilo.

Aliwataka maofisa wa TRA kujenga mahusiano mazuri kati yao, wafanyabiashara na wananchi ili kuondoa malalamiko yaliyopo ambapo alisema amekuwa akipata malalamiko mengi kuhusiana na misuguano iliyopo.

Kwa Wilaya ya Chunya zoezi la ulipaji wa kodi ya majengo ulianza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018.

**Sio kwamba wananchi hawataki kulipia kodi za majengo bali hawana elimu ya kutosha ni jambo geni kwao, tuendelee kuwafundisha taratibu wataelewa**





# Watishia kutoa shilingi bila gari la Mufti Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema Mufti Mkuu wa Zanzibar atapatiwa huduma za usafiri wa gari ambayo itamwezesha kufanya shughuli zake za kikazi kwa ufanisi mkubwa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia, alisema hayo baada ya kulazimika kutoa ufafanuzi kufuatia baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutishia kuzuia shilingi katika bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, kuhusu suala la muda mrefu la Mufti kupatiwa usafiri.

"Mheshimiwa nitazuia shilingi katika bajeti hii kama sitapewa ufafanuzi wa kina kwa nini hadi sasa Mufti ameshindwa kupatiwa usafiri wa uhakika kwa zaidi ya miaka mitano sasa," alisema Jaku Hashim Ayoub.

Akitoa ufafanuzi zaidi Balozi Ramia alisema tangu katika bajeti ya mwaka jana fedha zilitengwa kwa ajili ya kupata gari ya Mufti, lakini tatizo ikawa ni gari ya aina gani inayohitajika.

Alisema katika bajeti ya mwaka huu tayari fedha zimetengwa na kuongezwa zaidi na hivyo kazi iliyofanywa kwa sasa ni kutafuta gari yenye hadhi ambayo itatumiwa na kiongozi huyo wa dini ya Kiislamu.

Hata hivyo, alisema katika kipindi chote hicho kiongozi huyo alikuwa akitumia usafiri wa gari katika shughuli zake mbalimbali.

"Mheshimiwa matarajio yangu makubwa kwamba mwaka huu wa bajeti gari yenye hadhi kwa ajili ya Mufti Mkuu wa Zanzibar itapatikana...hata hivyo, Mufti kwa muda wote huo alikuwa ana usafiri ingawa wajumbe wengi walitaka gari yenye hadhi," alisema.

## Pemba yapata matumaini ya Jaji Mkaazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, amesema kufuatia kuongezeka kwa idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar yapo matumaini makubwa kwamba kisiwa cha Pemba kitapatiwa Jaji Mkaazi.

Mwalimu alisema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliokuwa wakijadili bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema idadi ya majaji imeongezeka kutoka wanne hadi kufikia tisa, huku wakiwapo watatu wanawake waliopo katika Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Alisema kilio cha kutaka kuwapo Jaji Mkaazi katika kisiwa cha Pemba ni cha muda mrefu kinachotokana na malalamiko ya wananchi kupitia wawakilishi wao.

Alisema serikali ilishindwa kupeleka Jaji Mkaazi katika kisiwa cha Pemba kutokana na uhaba wa majaji pamoja na mahakimu.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi kwamba tunajiandaa kupeleka Jaji Mkaazi ambaye atakuwa na jukumu la kusikiliza kesi ikiwamo za rufani," alisema.

Alisema jaji huyo kwa kiasi kikubwa atasaidia kusikiliza rufani kutoka kwa wafungwa waliopo katika Magereza mbalimbali ya Pemba na kusikilizwa kwa haraka.



Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Muhammed Raza (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Muhammed Said, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wingi wa talaka wamtisha Naibu Spika, aomba Mufti kutoa elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, ameitaka Ofisi ya Mufti kuendelea kutoa elimu ya ndoa ili kudhibiti tatizo la wingi wa talaka zinazotolewa kiholela na kusababisha wanawake kutelekezwa pamoja na watoto.

Mgeni alisema hayo wakati akichangia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kuwa Zanzibar inaongoza kwa wingi wa talaka katika nchi ziliopo Afrika ya Mashariki na Kati pamoja na wanaume kutelekeza watoto na mke.

Alisema elimu ya ndoa inahitajika ili kuwafanya watu wawili wenye nia ya kufunga ndoa kufahamu kila mmoja majukumu yake na haki na fursa zinazopatikana katika ndoa.

Mgeni alipongeza ofisi ya Mufti kwa kuanzisha madarasa ya ndoa ambayo huwakutanisha vijana wenye nia ya kufunga ndoa kwa kupata elimu kabla ya kuoana.

"Nimefurahishwa na kitendo cha ofisi ya Mufti kuanzisha madarasa ya ndoa ambayo lengo lake kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la talaka na kusambaratika kwa ndoa hizo katika kipindi kifupi," alisema.

Mgeni ambaye alipata kushiriki katika kufungua mafunzo ya darasa kwa wanandoa, alitaka madarasa hayo kuenea hadi vijijini kwa lengo la kufikisha elimu na kupunguza ndoa kusambaratika kiholela.

Aliishauri ofisi ya Mufti kuhakikisha elimu hiyo kufikishwa katika kila wilaya za Unguja na Pemba na kuwafikia walengwa wenye nia ya kufunga ndoa.

"Nimefurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na ofisi ya Mufti kufungua darasa kwa wanandoa na matarajio yangu elimu ya ndoa itafika vijijini," alisema.

Alitaka Sheria ya Mahakama ya Kadhi kuwabana zaidi wanaume wanaotelekeza wake na watoto na kusababisha familia kusambaratika.

Alisema wanaume wamekuwa wakitoa talaka kiholela kwa sababu sheria zilizopo haziwabani katika kutunza familia ikiwamo watoto.

"Sheria za Mahakama ya Kadhi bado zinahitaji marekebisho kwa sababu haziwabani wanaume wanaotoa talaka kiholea na matokeo yake ni kusambaratika kwa familia na kuzalisha watoto wa mitaani," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**PUBLICATION SUMMONS**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**
**(WITH EXTENDED JURISDICTION)**
**CRIMINAL APPEAL NO. 20/2020**
**(Arising from Criminal Case No. 404/2017 KARAGWE District Court)**
**DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION .........APPELLANT**
**VERSUS**
**JOVITHA CHARLES & I ..........RESPONDENTS**
**NOTICE OF HEARING**

**TO: JOVITHA CHARLES & I**

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for Hearing on the 20th day of MAY, 2020 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. J.D. LUAMBANO - RM. your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this **13th day of May, 2020.**

157446

PUBLICATION SUMMONS
IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA
(WITH EXTENDED JURISDICTION)
CRIMINAL APPEAL NO. 19/2020
(Arising from Criminal Case No. 37/2017 BIHARAMULO District Court)
DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION ..........................APPELLANT
VERSUS
JAMES MALIATABU ......................RESPONDENT

NOTICE OF HEARING

TO: JAMES MALIATABU

TAKE NOTICE that the mentioned case has been set down for Hearing on the 20th day of **MAY, 2020 at 8:30 O'clock** in the forenoon, Before Hon. J.D. LUAMBANO - RM. your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 13th day of May, 2020.

157446

PUBLICATION SUMMONS

IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA
(WITH EXTENDED JURISDICTION)
CRIMINAL APPEAL NO. 16/2020
(Arising from Criminal Case No. 154/2016 BUKOBA District Court)
DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION ..........................APPELLANT

VERSUS
RAHIMU KARIM & I ............RESPONDENTS

**NOTICE OF HEARING**

TO: RAHIMU KARIM
TAKE NOTICE that the mentioned case has been set down for Hearing on the 20th day of MAY, 2020 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. J.D. LUAMBANO - RM. your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 13th day of May, 2020.

157446

PUBLICATION SUMMONS
IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA
(WITH EXTENDED JURISDICTION)
CRIMINAL APPEAL NO. 11/2020
(Arising from Criminal Case No. 407/2016 KARAGWE District Court)
DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION ...........APPELLANT
VERSUS
MCHUNGUZI GREVAZ............................RESPONDENT

**NOTICE OF HEARING**

TO: MCHUNGUZI GREVAZ

TAKE NOTICE that the mentioned case has been set down for Hearing on the 20th day of MAY, 2020 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. J.D. LUAMBANO - RM. your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 13th day of May, 2020.

157446

PUBLICATION SUMMONS
IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA
(WITH EXTENDED JURISDICTION)
CRIMINAL APPEAL NO. 35/2020
(Arising from Criminal Case No. 40/2014 BUKOBA District Court)
DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION ......APPELLANT
VERSUS
KAMUGISHA PETRO.........................RESPONDENT

**NOTICE OF HEARING**

TO: KAMUGISHA PETRO

TAKE NOTICE that the mentioned case has been set down for Hearing on the 20th day of MAY, 2020 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. J.D. LUAMBANO - RM. your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 07th day of May, 2020.

157446

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Ibwera**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NO. 04/2020**

Ombi la Severine Gando kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Protase Rwiza Byarugaba.

Kwa kuwa Severine Gando ameomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Protase Rwiza Byarugaba, watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka, mnamo tarehe 26 mwezi 06/2020 kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo/ haupo mahakamani waweza/hauwezi kukaguliwa.

Tarehe 15/05/2020

157445

***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## China ni mapema uchunguzi virusi corona

**BEIJING,** China

WIZARA ya Mambo ya Nje ya China imesema ni mapema mno kuanzisha mara moja uchunguzi kuhusu kilikoanzia kirusi cha corona pamoja na kusambaa kwake.

Msemaji wa wizara hiyo, Zhao Lijian, aliwaambia waandishi habari wakati wa utoaji wa taarifa za kila siku kwamba nchi nyingi duniani zinaamini kwamba janga la mlipuko wa kirusi hicho halijamalizika.

Kufikia sasa zaidi ya watu 300,000 wamekufa duniani kutokana na kirusi hicho.

Wizara hiyo ya mambo ya nje ya China imefahamisha pia kwenye taarifa nyingine kwamba, Rais Xi Jinping, atatoa hotuba kwa njia ya video ya ufunguzi wa kikao cha baraza la Shirika la Afya Duniani, (WHO) siku hiyo. **DW**

## Kanisa la St. Peter Basillica lafungua milango yake

**ROME,** Italia

KANISA Kuu la Katoliki duniani la St. Petro lililoko Vatican nchini Italia, limefunguliwa jana kwa ajili ya wageni baada ya kufungwa kwa zaidi ya miezi miwili kutokana na sheria iliyotangazwa nchini humo ya vizuizi kwa lengo la kudhibiti kusambaa kirusi cha corona.

Wageni wachache walipanga foleni jana wakizingatia amri ya watu kutosogeleana karibu na kupimwa joto kabla ya kuingia ndani ya kanisa hilo huku polisi wakilinda.

Kanisa hilo lilifungwa tangu Machi 10, mwaka huu huku Italia ikiwa ni ya kwanza kufunga shughuli zote nchi nzima kwa zaidi ya miezi miwili iliyopita na kuufanya uchumi wa taifa hilo kuporomoka.

Kufikia sasa idadi rasmi ya waliokufa kutokana na kirusi hicho nchini humo ni watu 32,000. Makanisa yote mjini Rome yalifungwa mwanzoni mwa mwezi Machi. **DW**

# Hospitali za umma Brazil kuzidiwa wagonjwa corona

**BRASILIA,** Brazil

MEYA wa jiji kubwa zaidi nchini Brazil la Sao Paulo, Bruno Covas, amesema kuwa mfumo wa afya unaweza kuporomoka huku kukiwa na ongezeko la mahitaji ya vitanda vya dharura ili kuwahudumia wagonjwa wa corona.

Covas alisema hospitali za umma za jiji hilo zinaweza kujaa katika kipindi cha wiki mbili zijazo. Sao Paulo ni moja kati ya miji iliyoathirika zaidi nchini Brazil ambapo mpaka sasa watu 3,000 wamepoteza maisha kutokana na corona.

Jumamosi iliyopita, Brazil iliizidi nchi ya Uhispania na Italia na kuwa taifa la nne lenye idadi kubwa ya watu walioambukizwa corona.

Wizara ya Afya imeripoti maambukizo mapya 7,938 katika kipindi cha saa 24, jumla ya watu walioambukizwa ikifikia 241,000. Marekani, Urusi na Uingereza ndizo zilizo na idadi kubwa zaidi ya watu waliopata maambukizo.

**Rais wa nchi hiyo, Jair Bolsonaro, amekosolewa vikali ndani na nje ya nchi kwa namna anavyoshughulikia janga la corona linaloendelea kushika kasi.**

Idadi ya waliopoteza maisha katika nchi hiyo ya Amerika ya Kusini katika kipindi cha saa 24 ni watu 485, ikiwa na jumla ya vifo 16,118, takwimu zinazolifanya taifa hilo kushika nafasi ya tano kati ya nchi zenye idadi kubwa ya vifo.

Wataalamu wa afya nchini Brazil wameonya kuwa idadi kamili ya walioambukizwa inaweza kuwa kubwa zaidi kuliko takwimu zilizotolewa na serikali, kutokana na upungufu wa vipimo.

Rais wa nchi hiyo, Jair Bolsonaro, amekosolewa vikali ndani na nje ya nchi kwa namna anavyoshughulikia janga la corona linaloendelea kushika kasi.

Alipuuza ushauri wa wataalamu wa afya duniani kuhusu kutochangamana siku ya Jumapili alipopiga picha na watu wanaomuunga mkono na watoto katika mji wa Brasilia.

Covas alisema kuwa sasa yuko kwenye mazungumzo na Gavana wa Jimbo kuhusu hali hiyo kwa ajili ya kuweka marufuku ya kutotoka nje ili kujaribu kupunguza maambukizo kabla hospitali hazijazidiwa.

Gavana wa jimbo la Sao Paulo ana mamlaka kwa polisi, na msaada wake utakuwa muhimu ikiwa amri ya kutotoka nje itakuwa ya mafanikio.

Sao Paulo ina jumla ya watu karibu milioni 12, na takwimu zinaonesha kuwa wengi wa wakazi wa mji huo wamekuwa wakikiuka sheria ya kutochangamana.

Jimbo la Sao Paulo lilianzisha utaratibu wa karantini karibu miezi miwili iliyopita biashara, hospitali na maeneo ya umma yalifungwa na watu walitakiwa kukaa nyumbani.

Lakini hakuna adhabu yoyote kwa mtu atakayevunja sheria hizo. Wakazi wengi wa Sao Paulo wamekuwa wakiendesha magari mpaka kwenye fukwe za bahari wakati wa mwisho wa juma. **BBC**



Binti akielekezwa na mama yake namna ya kusafisha mikono katika kipindi hiki cha janga la virusi vya corona. **PICHA: MTANDAO**

# Marekani yapeleka ndege ya siri anga za juu

**WASHINGTON,** Marekani

JESHI la Anga la Marekani limefanikiwa kurusha roketi yake ya Atlas V katika anga za juu, huku ikiwa imebeba ndege aina ya X-37B itakayokwenda kufanya oparesheni za siri.

Roketi hiyo ilirushwa juzi kutoka eneo la Cape Canaveral, ikiwa ni siku moja tangu kuahirishwa kurushwa kutokana na hali mbaya ya hewa.

Ndege hiyo ambayo pia inajulikana kama Orbital Test Vehicle (OTV), itatuma satelaiti katika mzingo wa dunia (orbit) na kujaribu teknolojia mbalimbali katika eneo hilo la anga za mbali.

Hii ni safari ya sita ya kiuchunguzi kwa ndege hiyo katika anga za mbali.

Safari ya wakati huu imetunukiwa kwa wafanyakazi walio mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya virusi vya corona pamoja na walioathirika na virusi hivyo.

Ujumbe maalumu uliojumuisha maneno "Marekani ni thabiti" yaliandikwa kwenye kichwa cha roketi.

X-37B ni mradi maalumu wa siri ambao ni vitu vichache tu kuuhusu vinavyojulikana. Makao Makuu ya Jeshi la Marekani, Pentagon, yametoa maelezo machache kuhusu uwezo wa ndege hiyo isiyo na rubani.

"Oparesheni hii ya X-37B itafanya majaribio mengi zaidi kuliko oparesheni nyingine yoyote ya awali," Waziri wa Jeshi la Anga, Barbara Barrett, alieleza mwanzoni mwa mwezi huu.

Moja ya majaribio yatakuwa ni athari ya mionzi kwa mbegu na vitu vingine.

Programu ya X-37B ilianza mwaka 1999. Ndege hiyo inafanana na ndege ndogo ambazo zilikuwa zikirushwa na binadamu katika anga za mbali ambazo zilistaafishwa rasmi mwaka 2011.

Inaweza kurejea duniani kwa kushuka taratibu na kutua katika kiwanja cha ndege.

Ndege hiyo imetengenezwa na kampuni ya Boeing na inatumia umeme wa nguvu ya jua. Ina urefu wa futi 29 (sawa na mita 9), urefu wa mabawa yake ni takribani mita 15 na ina uzito wa kilo 4,989 (tani 4.9).

Kwa mara ya kwanza ndege hiyo iliruka angani mwezi Aprili 2010 na kufanya operesheni yake katika anga za juu kwa miezi minane.

Safari ya mwisho ya ndege hiyo (kabla ya hii mpya) ilifikia tamati mwezi Oktoba 2019, baada ya kukaa katika anga za juu kwa siku 780.

Kwa ujumla mpaka sasa ndege hiyo imeshatumia muda wa zaidi ya miaka saba kufanya operesheni zake za siri katika anga za mbali.

Haijulikani kwa safari hii ndege hiyo itachukua muda gani kumaliza operesheni yake. **BBC**




# WAKALA AKANUSHA SALAH KUPEWA OFA MADRID

**LIVERPOOL,** England

WAKALA wa nyota wa Liverpool, Mohamed Salah amekanusha madai kuwa alizungumza na kocha wake wa zamani kwamba, Real Madrid walijaribu kutuma ofa ya kumsajili mshambuliaji huyo mwaka 2018.

Nyota wa zamani wa Misri, Hany Ramzy, alisema Jumamosi kwamba, Salah alizungumza kuhusu kutakiwa na Madrid na kocha wa timu ya taifa wa wakati huo, Hector Cuper wakati wa mazoezi nchini Uswisi kuelekea Kombe la Dunia nchini Urusi.

Ramzy aliiambia televisheni moja ya nchini Misri ya OnTimes Sports kwamba alikuwapo wakati wawili hao wakizungumzia jambo hilo.

Lakini wakala wa Salah, Ramy Abbas Issa, amepuuzia madai hayo kupitia mtandao wa Twitter.

"Mohamed hajawahi kuzungumza mipango yake na kocha wake wa zamani," aliandika.

Salah alifurahia msimu bora wa 2017-18, akifunga mabao 32 kwenye Ligi Kuu na kutoa pasi za mwisho 10.

Vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp wakafungwa 3-1 kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid msimu huo, huku Salah akitolewa nje dakika za mwanzo baada ya kuchezewa rafu na Sergio Ramos.

Salah amefunga mabao 91 katika mechi 144 tangu alipowasili Liverpool akitokea AS Roma mwaka 2017.




# Barca wasimsajili tena Neymar- Elber

**SAO PAULO,** Brazil

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Brazil, Giovane Elber anahisi Barcelona hawatakiwi kumsajili tena Neymar, wakati akihoji maamuzi ya mshambuliaji huyo kujiunga na Paris Saint-Germain.

Neymar mwenye umri wa miaka 28, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Barca, karibia miaka mitatu baada ya kujiunga na PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222.

Lakini Elber, ambaye alitamba akiwa Bayern Munich na kucheza mechi 15 kwa timu ya taifa ya Brazil, amesema miamba hao wa LaLiga hawatakiwi kumchukua tena Neymar ili arudi pale Camp Nou.

Akiwa ameulizwa na televisheni ya Cadena SER kama Barca wanatakiwa kumsajili tena Neymar, Elber alisema: "Hapana. Namna alivyoondoka Barcelona, kwa upande wangu hakuna uwezekano wa kurudi Barcelona."

Elber aliongeza: "Kwa upande wangu, Neymar hakuwa na tabia nzuri pale Barca, kwa sababu wakati alipotaka kuondoka Barcelona alisema anataka kuwa bora duniani.

"Lakini nje ya uwezo wa Mungu, huwezi kuwa bora duniani kwa kuichezea PSG. Kwa hilo unatakiwa kwenda Real Madrid au Barcelona, kwenye timu ambayo unaweza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Naamini PSG haitakuwa na uwezo wa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka mitatu au minne ijayo."

# Nani na stori ya Ferguson

**MANCHESTER,** England

NANI amekiri kwamba, alikuwa "mwoga sana" kwa Alex Ferguson wakati alipowasili kwa mara ya kwanza pale Manchester United, akielezea namna alivyopata wakati mgumu kumwendesha kwenye gari wakati wakirudi nyumbani siku moja.

Nani alihamia pale Old Trafford kutoka Sporting CP mwaka 2007 na akashinda mataji manne ya Ligi Kuu na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini raia huyo wa Ureno amesema awali alikuwa anamuogopa Ferguson, ambaye tayari alikuwa ameinoa United kwa zaidi ya miaka 20.

"Mwanzoni, nilikuwa namuogopa sana. Kama baba, unajua? Kufanya kosa au kitu chochote tofauti, kwa sababu wakati mwingine nilikuwa nashindwa hata namna ya kuzungumza naye," alisema Nani, ambaye kwa sasa anaichezea klabu ya Orlando City, akiiambia UTD Podcast.

"Nilikuwa namuona anazungumza na wachezaji wengine na nilitaka kujiunga nao, lakini nilikuwa nafikiria nitakwenda kusema nini, unajua? Sikujua. Lakini nilikuwa namuogopa hadi nilipojifunza namna ya kumuelewa na kuweza kujieleza mimi mwenyewe.

"Kiingereza changu hakikuwa sawa, au hakitakuwa sawa, lakini kipindi kile kilikuwa kibaya sana na wakati nilipogundua naweza kuzungumza naye zaidi, alianza kuja na kunisikiliza mimi. Na halafu kuanzia hapo, nikajifunza mengi kuhusu Sir Alex Ferguson. Nini alichokuwa anataka kifanyike, namna alivyo na mahusiano yangu yakaanza kuwa mazuri.

"Yeye ni mtu ambaye anajua namna ya kuishi na watu wote, wenye umri tofauti, wenye tabia tofauti. Kipindi kile nilikuwa mdogo kiumri, na haikuwa rahisi. Najua kwamba nilijifunza mengi, nilibadilika sana. Ndio maisha yalivyo. Unatakiwa kujifunza."

Bado, Nani anakumbuka wakati alipomwendesha kwa gari Ferguson kurudi nyumbani wakati walipotoka sare ya kufungana 2-2 ugenini na Fulham Agosti 2010.

Nani alitokea benchi na kukosa penalti, ambayo alipiga yeye badala ya mpigaji wa mara kwa mara, Ryan Giggs.



HABARI MICHEZO

# Neuer aikana Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

MANUEL Neuer amekanusha madai ya Karl-Heinz Rummenigge kwamba anakaribia kusaini mkataba wa kuongeza muda hapo Bayern Munich.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Neuer mkataba wake na Bayern unamalizika msimu ujao na mazungumzo ya kuongeza mpya yamesimama.

Golikipa huyo mwenye umri wa miaka 34, mwezi uliopita alikanusha ripoti kwamba anataka mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya euro milioni 20 kwa mwaka na kuonyesha kukasirishwa kwake na kuvujishwa kwa taarifa hizo kwenye vyombo vya habari.

Bayern kwa sasa wapo kwenye mpango wa kumsajili kipa Alexander Nubel kutoka Schalke mwishoni mwa msimu huu, lakini Rummenigge bado anajiamini watafikia makubaliano na Neuer.

"Nina uhakika kwamba Manuel hivi karibuni ataikubali ofa ya FC Bayern," alisema Mwenyekiti wa Bayern, Rummenigge akiiambia Sky Sport baada ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Union Berlin Jumapili, mchezo huo ukiwa wa kwanza tangu Bundesliga ilipositimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Manuel Neuer anajua nini alichonacho pale FC Bayern na FC Bayern wanajua nini alichonacho Manuel Neuer. Kwa hiyo, ni ndoa ambayo itaendelea kwa siku za usoni."

Hata hivyo, Neuer alitoa taswira tofauti kabisa baada ya mchezo huo.

Alisisitiza kwamba bado hajafikia makubaliano ya kuongeza mkataba, lakini bado anaamini wanaweza kuafikiana.

"Nafikiri Karl-Heinz Rummenigge anajua nini kinachoendelea. Hakuna cha kutangaza kwa sasa," alisema Neuer.






# IBRAHIMOVIC AKATALIWA BOLOGNA

**ROME,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Bologna msimu ujao, lakini Mkurugenzi wa klabu hiyo, Walter Sabatini amemwagia maji ya baridi wazo hilo.

Kocha wa Bologna, Sinisa Mihajlovic wikendi hii alisema Ibrahimovic, alimuambia anaweza kuondoka Milan baada ya msimu huu wa 2019-20.

Mihajlovic alidai mshambuliaji huyo mkongwe uhamisho wake ujao utakuwa kati ya kurudi Sweden au kujiunga na Bologna, lakini Sabatini anafikiri mpango huo uko mbali.

"Ni jambo ambalo linaweza kuwa kwenye mahusiano yao tu ya kirafiki," alisema Sabatini akiiambia Sky Sport Italia.

"Uhamisho wa kumhusisha Ibrahimovic si kitu ambacho Bologna wanaweza kukifikiria kwa sasa.

"Ni jambo la kushangaza, kwani hakuna kinachowezekana kwa sasa, lakini siwezi kuamini kwamba kitu hiki kinaweza kutokea."

# *Rooney: Utd walikosea kumtimua Van Gaal*

**MANCHESTER,** England

WAYNE Rooney anahisi Manchester United walikosea kumfukuza Louis van Gaal mwaka 2016 baada ya miaka miwili ya kukaa pale Old Trafford.

Van Gaal alifukuzwa na nafasi yake akapewa Jose Mourinho muda mfupi baada ya kushinda taji la FA, huku United wakiwa wameamaliza nje ya nne bora kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

Chini ya Mourinho, United ilimaliza nafasi ya sita kwenye msimu wa 2016-17, lakini walishinda mataji mawili ya EFL na Ligi ya Europa.

Bado Rooney, ambaye wakati huo alikuwa nahodha wa United, amesisitiza klabu ilitakiwa kumpa angalau mwaka mmoja Van Gaal kuthibitisha mafanikio yake.

"Nilishtuka wakati Louis alipofukuzwa," alisema Rooney katika Kitabu cha 'LVG - The Manager and the Total Person'.

"Kwa upande wangu, nilifurahia sana kufanya naye kazi.

"Tulitakiwa kumbakisha kwa mwaka wa tatu. Tungekuwa imara zaidi.

"Nahisi mambo yangeimarika zaidi na wachezaji walianza kuelewa mtazamo wake. Kwa miaka ile miwili tayari nilishajifunza mengi zaidi nikiwa chini yake kuliko kwa mwingine yeyote."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI ATAKIWA KUIPIKU REKODI YA MULLER

**Ni ile ya kufunga mabao 40 kwa msimu mmoja wakati huu akiwa ameshaziona nyavu mara...**

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski amepewa changamoto ya kufikia rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao 40 kwa msimu mmoja wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Raia huyo wa Poland amefikisha mabao 26 msimu huu katika mechi 24 za Ligi pamoja na kutengeneza penalti ya juzi Jumapili iliyoiwezesha Bayern kupata ushindi wa 2-0 dhidi ya Union Berlin.

Ukiwa ni mchezo wao wa kwanza baada ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Bayern walitawala mchezo huo, ingawa hawakuwa kwenye kiwango chao bora.

**Na Kocha Mkuu wa Bayern, Hansi Flick ambaye anategemea mabao ya nyota huyo, anaamini bado kuna mengi yanakuja kutoka kwa Lewandowski.**

Bayern imebakiwa na mechi nane kumaliza ligi na hivyo Lewandowski atatakiwa kupambana sana ili kuifikia rekodi ya Muller, ambaye aliweka klabu hapo msimu wa 1971-72.

Flick anaona hilo linawezekana kwa Lewandowski na kusema: "Lewy yupo kwenye kiwango cha kuvutia, nafikiri anaweza kuifikia.

"Amefunga mabao 26 na mechi nane zimebakia ili kuvunja rekodi ya Gerd Muller. Haitakuwa kazi rahisi, lakini ana ubora huo. Kama kuna mtu anaweza kuifikia basi ni yeye.

## ZISIKUPITE

### GREALISH AKOMALIWA UTD

KLABU ya Manchester United itatakiwa kulipa pauni milioni 80 kwa kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24, hataka kama timu yake itashuka daraja kutoka Ligi Kuu ya England. ***(Mirror)***

### JUVE BADO INAYE JIMENEZ

JUVENTUS itapambana na Manchester United kwenye mbio za kumsajili mshambuliaji wa Wolves, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29. ***(Times)***

### FRASER KUTIMKIA SPURS

WINGA wa Bournemouth na Scotland, Ryan Fraser mwenye umri wa miaka 26, inaaminika anataka kujiunga na Tottenham Hotspur kwa uhamisho huru wakati mkataba wake utakapomalizika pale Cherries Juni 30. ***(Mirror)***

### TOLLISSO ATAKIWA UNITED

KIUNGO wa Bayern Munich, Corentin Tolisso anawaniwa na Manchester United na klabu hiyo ya Ujerumani ipo tayari kumuachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 raia wa Ufaransa, ili aweze kupata fedha za kununulia wachezaji wengine, akiwamo winga wa Manchester City na Ujerumani, Leroy Sane mwenye miaka 24. ***(Express)***

### LIVERPOOL YATUA ROMA

KLABU ya Liverpool inafikiria kumsajili mshambuliaji wa AS Roma, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 20, katika kipindi cha majira ya joto, ambaye anawaniwa na klabu za Manchester United na Tottenham. ***(Corriere dello Sport - via Sports Mole)***

### LLORENTE KUTIMKA SOCIEDAD

BEKI wa Real Sociedad, Diego Llorente mwenye umri wa miaka 26, anaangalia uwezekano wa kuhama kipindi cha majira ya joto kinachokuja na Monaco na Liverpool ni miongoni mwa klabu zinazomuwania. ***(La Razon)***

### UTD KUKAZA KWA SKRINIAR

MANCHESTER United italazimika kuzima mpango wa Real Madrid kwa mlinzi Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, huku Inter Milan ikijiandaa kumwachia kuondoka kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Mirror)***

### KOFFI HAJUTII KUIKATAA

KIUNGO wa Fiorentina, Christian Koffi mwenye umri wa miaka 19, aliamua kutojiunga na Liverpool mwaka 2018, lakini amesema hakufanya kosa. ***(So-foot)***

### TONALI HUYO INTER MILAN

KIUNGO wa Brescia, Sandro Tonali, ambaye amekuwa akihusishwa na kutakiwa na Liverpool, anaelekea kujiunga na Inter Milan baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, kukataa uhamisho wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus. ***(Le10 Sport)***

### CHIRIVELLA HAJAAMUA LIVER

KIUNGO wa Liverpool, Pedro Chirivella mwenye umri wa miaka 22, amepewa ofa ya miaka mitano, lakini bado hajaamua kuhusu majaliwa yake ya baadaye, akiwa pia amepata ofa kutoka Nantes na Rangers. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Ndayiragije atetea wachezaji Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amefunguka na kuitaka Bodi ya Ligi (TPLB), kutoa muda wa wiki tatu wachezaji kupata muda wa kujiandaa kabla ya Ligi Kuu kuanza rasmi, endapo serikali itaruhusu michezo kuendelea nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Ndayiragije (pichani) alisema angalau Shirikisho la Soka nchini (TFF) na TPLB wangewapa wiki tatu wachezaji na klabu zao ili kujiweka fiti kabla ya kurejea uwanjani.



"Wachezaji wangepewa wiki tatu za kujiandaa ili kujiweka sawa kabla hawajaanza majukumu zitawasaidia kwa kiasi kikubwa," alisema.

Vile vile alisema inapaswa kupewa muda huo kwa wachezaji kukaa pamoja katika mazoezi kwa kile alichodai kila mchezaji alipewa programu yake ya mazoezi na kocha, hivyo ni vema kwa kocha kupata muda wa kuwaunganisha upya.

"Kipindi chote cha mapumziko kila mwalimu alitoa maelekezo kwa wachezaji wake na maelekezo si rahisi kuwa sawa kuna kila sababu kuwaweka pamoja kwa muda mrefu kabla ya kuanza kucheza," alisema.

## Manara aonya Ligi Bara ikirejea

**Na Saada Akida**

MKUU wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Hajji Manara, amewataka wadau wa soka kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, pindi Ligi Kuu Bara itakaporejea.

Manara ametoa kauli hiyo, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Dk. John Magufuli, juzi kusema kama hali ya maambukizo ya virusi vya corona itaendelea kuwa ya chini kama ilivyo sasa, ataruhusu ligi nchini kurejea hata wiki hii.

"Kauli ya mheshimiwa rais kurejesha ligi haina maana tusichukue tahadhari juu ya janga hili, hivyo tutakaporejea tunatakiwa kuzingatia maelekezo ya mamlaka husika juu ya kuchukua tahadhari ya kujilinda na ugonjwa huu," alisema Manara.

Alisema wamepata faraja kubwa na kauli hiyo wakiwa kama wadau wa soka na wameipokea kwa furaha kubwa, lakini rais amelisaidia Shirikisho la Soka nchini (TFF) kutua mzigo mkubwa juu ya nani ataiwakilisha nchini katika michuano ya kimataifa endapo ligi ingefutwa.

"Nadhani hili TFF hawajaliweka wazi, ila kwa utamaduni wetu Tanzania ingekuwa maneno kuwa Simba imebebwa endapo ingepewa nafasi hiyo kama ilivyo kwa mataifa mengine kuwapa nafasi timu inayoongoza ligi au bingwa mtetezi," alisema.

# AZAM SHANGWE MAGUFULI KURUHUSU NDEGE KUTUA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umesema wamepata faraja baada ya kusikia kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dk. John Magufuli ya kufungua viwanja vya ndege nchini kwa kuruhusu ndege kutoka nje kutua.

Ofisa Habari wa Azam FC, Zaka Zakazi, jana alisema kitendo cha Rais kufungua viwanja vya ndege kimewafurahisha kwa sababu sasa wanaimani wachezaji wao wa kulipwa saba pamoja na makocha walioko makwao watarejea nchini.

"Kutangazwa ligi kurejea, tulishafurahi tangu rais aliposema wiki moja iliyopita katika hotuba yake ya awali, ila lililotufurahisha zaidi jana [juzi]ni kuhusu kufungua viwanja vya ndege nchini.

**"Ukizingatia nyota wetu hao saba na makocha wote walikwama kurejea baada ya viwanja vya ndege kufungwa kutokana na janga hili la corona, kwa kauli ya kufungua viwanja inatupa matumaini ya wao kurejea," alisema Zaka.**

Alisema wana imani nyota hao watarejea mapema kabla ya kurejeshwa kwa Ligi Kuu Bara.

Aliwataja wachezaji ambao walikwama kurejea kutokana na sakata hilo kuwa ni Razak Abalora, Yakub Mohammed, Daniel Amoah (Ghana), Nicholas Wadada (Uganda), Never Tigere, Donald Ngoma na Bruce Kangwa (Zimbabwe) pamoja na Kocha Mkuu, Mromania Aristica Cioaba na msaidizi wake, Mrundi Vivier Bahati.

"Endapo Ligi ingerejea huku viwanja vya ndege vikiwa vimeendelea kufungwa tungeathirika kwa kuwakosa nyota hao pamoja na makocha wetu," alisema Zaka.

MILIKI...



Wachezaji wa timu ya Fedha FC, wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Kaheza awazia soka la kimataifa*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Polisi Tanzania, Marcel Kaheza, amesema bado anafikiria kucheza tena soka nje ya nchi, licha ya kurejea nchini akitokea Kenya ambako alikuwa akicheza soka la kulipwa kwenye klabu ya AFC Leopards ya Kenya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Kaheza anayeichezea timu hiyo kwa mkopo akitokea Simba, amesema mkataba wake na Polisi Tanzania unamalizika mwishoni mwa msimu huu na sasa kama si kubaki na timu hiyo, basi ataangalia changamoto nyingine nje ya nchi.

"Ni kweli kwa sasa namalizia mkataba wangu, tayari nina mazungumzo na timu yangu ya Polisi Tanzania kama wakifanikisha kunibakisha, lakini kama sivyo, basi siangalii hapa, naangalia nafasi nyingine ya kwenda kucheza soka la kulipwa," alisema mchezaji huyo ambaye Simba ilimsajili akitokea Majimaji ya Songea.

Straika huyo ambaye kwa sasa ana mabao sita Ligi Kuu, aliongeza: "Bado nina umri mdogo na ndoto zangu ni kutoka hapa na kwenda kucheza soka kwenye klabu mbalimbali kubwa barani Afrika na kwingineko, uzuri ni kwamba tayari nimeshatoka kucheza soka nje ya nchi, najua changamoto za huko, hivyo nitakabiliana nazo," alisema.

Kaheza ambaye alianzia soka kwenye kikosi cha vijana cha Simba kabla ya kwenda Majimaji ya Songea, alisajiliwa tena na Simba mwaka 2018, lakini kutokana na wakati huo klabu hiyo kuwa na malengo makubwa zaidi kwa kusajili wachezaji kama Meddie Kagere, Claotus Chama na wengine, alikosa nafasi na mwaka huo huo akapelekwa klabu ya AFC Leopards ya Kenya kwa mkopo.

Mwaka mmoja baadaye alirejea nchini na kujiunga tena kwa mkopo klabu ya Polisi Tanzania ambayo anamaliza mkataba wake pindi Ligi Kuu Tanzania Bara itakapomalizika, hivyo kuwa na uhuru wa kuchagua kituo kingine kiwe ndani ama nje ya Tanzania.

Michezo

Jumanne Mei 19, 2020

Nipashe



Lewandowski atakiwa kuipiku rekodi ya Muller UKURASA 22

SUBIRINI...




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe. **PICHA: MAKTABA**

# Takukuru: Watazitapika fedha za JPM Afcon U-17

## ●●● Waziri Mwakyembe asema Rais wa TFF hawezi kujiweka kando, amtaka kutoa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), ikisema waliotafuna fedha zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli lazima wazitapike kama ambavyo alionya wakati akizitoa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amesema Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia hawezi kujiweka kando katika sakata hili.

**Rais Magufuli alitoa fedha hizo kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika kwa Vijana chini ya umri wa miaka 17 (Afcon U-17), yaliyofanyika nchini Aprili mwaka jana na wakati akitoa alionya endapo zitatumika ndivyo sivyo walaji watazitapika.**

Hata hivyo, Takukuru imeeleza kulikuwa na upigaji katika fedha hizo, jambo ambalo imelifanya kuingia kazini kuchunguza huku ikiwataka waliozichota kuzirejesha mapema.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kupitia kituo kimoja cha redio nchini, Waziri Mwakyembe alisema TFF inapaswa kupeleka ushahidi Takukuru na si kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kujitetea na kwamba kwa kufanya hivyo si sahihi kwa sasa kwa sababu taasisi hiyo tayari imeanza uchunguzi.

Dk. Mwakyembe alisema katika sakata hili Karia hawezi kujiweka kando kwa kuwa yeye aliingia moja kwa moja katika kamati ya maandalizi ya ndani (Local Organizer Committee) za fainali hizo, hivyo kinachotakiwa kwake na shirikisho hilo ni kutoa ushirikiano kwa Takukuru ili iweze kufanya kazi yake.

Aidha, Dk. Mwakyembe alisema vyombo vya habari vinapaswa kuwa makini katika kuripoti suala hilo kwa kuwa hata fedha zinazochunguzwa si Sh. bilioni moja kama ambavyo vinaripoti kwa kuwa kiasi kilichopokelewa kilikuwa zaidi ya Sh. bilioni 1.7.

"Kuhusu hela msipotoshe mjadala zilikuwa zaidi ya Sh. bilioni 1.7, iacheni Takukuru ifanye kazi yake, wasaidieni Takukuru kama kuna kitu pelekeni huko, niwaombe wote hata BMT [Baraza la Michezo Tanzania] nao kama wana kitu wapeleke huko," alisema waziri huyo mwenye dhamana na michezo nchini.

Alisema mbali na Sh. bilioni moja iliyotolewa na Rais Magufuli, zipo fedha zingine kutoka kwa wadau mbalimbali waliochangia katika kufanikisha maandalizi ya michuano hiyo iliyofanyika kwa mara ya kwanza nchini.

Alipoulizwa Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia John Mbungo, alisema bado wanaendelea na uchunguzi na taasisi hiyo haitabakiza kitu na kwamba waliozitafuna lazima wazitapike kama ambavyo Rais Magufuli alitamka wakati akizitoa.

"Bado tupo kwenye uchunguzi, tuacheni kwanza kwa sababu kwa sasa kila mtu ataongea chake, kila kitu lazima kichunguzwe, hatutabakisha kitu lazima wazitapike kama ambavyo rais alisema, sisi tumewaagiza wazirudishe hizo fedha," alisema.

Kadhalika, Mbungo naye alieleza fedha zinazochunguzwa ni zaidi ya Sh. bilioni moja kwa kuwa wapo wadau mbalimbali walitoa michango yao ili kufanikisha fainali hizo likiwamo Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Wiki iliyopita Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema fedha hizo zilikuwa chini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ndani ambaye alikuwa Waziri Mwakyembe na makamu wake, Mwenyekiti wa BMT, Leodegar Tenga.

"Fedha kupokelewa na matumizi yake, yalikuwa yanasimamiwa na vyombo vinavyohusika na wizara yenye dhamana ya michezo, sisi kama TFF, fedha hatukupata kupitia kwetu, zilipitia katika mamlaka nyingine ili kufanikisha mashindano yanayofanyika," alisema Kidao.

# TFF kukwepa ratiba EPL Ligi Kuu ikirejea

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, akieleza kuwa endapo hali ya maambukizo ya virusi vya corona itaendelea kuwa chini kama ilivyo kwa sasa ataruhusu michezo kurejea hata wiki hii, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limesema kabla ya Ligi Kuu kuanza itabidi kuimulika kwanza ratiba ya Ligi Kuu England (EPL) ili kuikwepa.

Juzi Rais Magufuli alieleza kufurahishwa na takwimu za wagonjwa wa corona nchini kupona na kuahidi kama hali ikiendelea kuwa hivyo, ataruhusu vyuo kufunguliwa pamoja kuruhusu michezo iendelee maana ni moja ya burudani kwa Watanzania.

Hata hivyo Rais wa TFF, Wallace Karia, akizungumza na BBC Redio jana, alisema kama serikali ikitoa baraka ya ligi kurejea watahakikisha wanatoa muda wa kutosha kwa timu kujiandaa na ligi hiyo kurejea katikati ya Juni, lakini itabidi kuichunguza kwanza ratiba ya Ligi Kuu England ambayo nayo inatarajiwa kuanza mwezi ujao ili kukwepa mwingiliano.

"Watanzania wanapenda sana Ligi Kuu England, hivyo kama serikali ikiruhusu ligi kurejea, itabidi kuangalia ratiba ya England ili kuzipishanisha na Ligi Kuu Bara, kutoa nafasi kwa mashabiki kuona mechi zote kwa kuwa watakuwa wanaishuhudia kupitia TV," alisema Karia.

Kuhusu afya za wachezaji, alisema wamejipanga kuchukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kushiririsha kamati zote za afya pamoja na wizara husika kwa kuwa TFF inatanguliza kwanza afya za wachezaji mbele pamoja na mashabiki wake.

"Kwanza wachezaji wote watapimwa na tutatoa muda wa kujiandaa, lakini mashabiki hawataruhusiwa kuingia uwanjani watashuhudia kupitia TV, na watakaoruhusiwa ni viongozi wa timu na waandishi wa habari wachache, na tutashirikiana kwa karibu katika kuchukua tahadhari na kamati zetu zote za afya pamoja na Wizara ya Afya," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >